Nipashe
Jumanne Mei 26, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580241
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
MWANGA WA JAMII




UKURASA 11



## Kesi mbunge, 'house boy' yaanza kunguruma kortini

UKURASA 4

# Msajili avipa utaratibu vyama kuelekea Oktoba

**AVIKUMBUSHA** mambo muhimu ya kuzingatia kwenye mchakato wa uchaguzi mkuu...*Endelea ukurasa 2*



Wakazi wa Kitunda Kivule nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, wakichuna mbuzi kwa ajili ya kitoweo cha Sikukuu ya Eid El Fitri, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## BAA LA CORONA



Wakati wa kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona, inashauriwa kuweka salama vifaa unavyofanyia kazi ofisini na nyumbani kwa kuvisafisha na dawa kama milango, vitasa vya madirisha na milango, jikoni, maliwato, vifaa kama simu, kompyuta na sehemu unayoweka vifaa hivyo. WHO

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## MASHIRIKA 8 NDEGE ZA NJE KUANZA SAFARI

UKURASA 4

# Polisi Dar walivyowaua watuhumiwa 7 ujambazi

UKURASA 2





Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store


MICHEZO SIMBA KAMILI KWA UBINGWA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Msajili avikumbusha vyama vya siasa kuelekea uchaguzi

**Na Salome Kitomari**

MSAJILI wa vyama vya siasa, Jaji Francis Mtungi, amevikumbusha vyama vya siasa kukabidhi ratiba zake za mchakato wa mambo mbalimbali wanapoelekea kwenye uchaguzi mkuu.

Akizungumza na Nipashe, alisema kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa vinapaswa kumshirikisha Msajili kwenye ratiba zao ndani ya vyama kuhusu mchakato wa uchaguzi.

Alisema hadi sasa hakuna mabadiliko ya Uchaguzi Mkuu na kwamba licha ya uwapo wa ugonjwa wa corona, shughuli zitaendelea kama kawaida, lakini kwa tahadhari kubwa.

"Tulishawaandikia (vyama) kwa mujibu wa sheria ya vyama vikifikia kwenye mchakato wa uchaguzi wakumbuke kutupatia ratiba zao," alisema.

"Hatuvizii (vyama) ili wakosee bali tunawakumbusha mapema kuweka wazi ratiba zao ili nasi tushiriki...wakienda kinyume tumepewa nguvu kisheria kuweka pingamizi," alibainisha.

Hivi karibuni, vyama vya CCM, Chadema na ACT Wazalendo, vilitangaza kuanza michakato ya ndani kuelekea uchaguzi mkuu ambao umebakisha miezi mitano na siku tano.

Majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ni kusajili chama cha siasa kinachokidhi vigezo vya usajili kwa mujibu wa sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 1992, ikiwamo kufuta chama chenye usajili wa muda au kudumu ambacho kwa mujibu wa sheria kimepoteza sifa ya usajili.

Vile vile, kifungu kidogo (1) cha (20) cha sheria ya vyama vya siasa kinamtambua Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa ndiye mwenye mamlaka ya kisheria anayeweza kusajili na kufuta usajili wa chama chochote cha siasa, uamuzi wake ni wa mwisho na hauwezi kukatiwa rufani.

Pia, amepewa mamlaka ya kusajili na kuvifuta vyama vinavyokiuka masharti ya usajili kwa mujibu wa sheria.

Majukumu mengine ni kuratibu shughuli za Baraza la vyama vya siasa, kufuatilia mapato na matumizi ya vyama vya siasa katika uchaguzi kwa mujibu wa Sheria ya gharama za uchaguzi ya mwaka 2010.

Mengine ni kufuatilia utendaji wa vyama vya siasa kwa mujibu wa sheria, kugawa ruzuku kwa vyama vya siasa vyenye sifa, kuwa kiungo kati ya serikali na vyama vya siasa nchini.

Pia, kutoa elimu kwa umma kwa vyama vya siasa na wadau wa vyama vya siasa.

Kwa mujibu wa tovuti ya Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, kuna vyama 19 vyenye usajili wa kudumu.

Kwa mujibu wa Katiba na ratiba iliyotolewa na Bunge hivi karibuni, Rais anaratajia kuvunja Bunge Juni 19, mwaka huu, huku uchaguzi Mkuu ukifanyika Oktoba 25, mwaka huu.

Licha ya mchakato wa ndani ya vyama baada ya Bunge kuvunjwa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), itatangaza ratiba ya uchaguzi mkuu ikiwamo kupiga kipyenga cha

Hata hivyo, kabla ya kuanza kwa kampeni, kutakuwapo na mchakato wa kuwawekea mapingamizi wagombea ambao wataonekana kutokuwa na sifa kisha NEC kutafanyia uamuzi kisha kufanya uteuzi wa mwisho wa wagombea watakaopeperusha bendera za vyama vya siasa vitakavyoshiriki katuika uchaguzi huo.



Katibu wa Ushirika wa Mama wa Kikristo (UMAKI) wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Magreth Massawa (kushoto), akitoa elimu ya kujikinga na virusi vya corona kwa wazee wa kijiji cha Sukamahela Wilaya ya Manyoni, mkoani Singida jana. Katikati ni Rhoda Mwaja na Julita Mapogo. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Kortini kesi uhujumu uchumi mil. 158/-

**Na Hellen Mwango**

MFANYAKAZI wa Kampuni ya Glotel Ltd, Jousia Msophe (32), mkazi wa Kigamboni, jijini Dar es Salaam, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu akikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo wizi wa kuaminiwa na kutakatisha Sh. milioni 158.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashitaka yake mwishoni mwa wiki iliyopita mbele ya Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Faraji Ngukah, alidai kuwa kati ya Juni Mosi na Septemba 26, 2019 mshitakiwa aliiba Sh. milioni 158 kutoka kwenye kampuni ya Glotel Ltd.

Ilidaiwa kuwa mshitakiwa aliiba fedha hizo ambazo alipewa na kuaminiwa kwa ajili ya biashara.

Ilidaiwa kuwa, Msophe alijipatia fedha hizo huku akijua kuwa ni zao la kosa tangulizi la wizi wa kuaminiwa.

Mshitakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.

Upande wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa Juni 4, mwaka huu na mshitakiwa apelekwe rumande.

# Polisi yaua majambazi saba wakijaribu kupora

**Na Romana Mallya**

WATU saba wanaosadikika kuwa majambazi wameuawa na polisi jijini Dar es Salaam na kufanikiwa kupata bastola aina ya Beretta ikiwa na risasi tatu.

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliwaambia waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea saa 6:10 usiku wa kuamkia jana maeneo ya Mwenge Coca Cola.

Kamanda Mambosasa aliwataka watu wenye ndugu yao ambaye hajarudi nyumbani jana, waende Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), kutambua miili.

"Mpaka sasa sina majina ya wahusika waliouawa ila kama una ndugu jambazi haonekani, alikwenda kuvuna akashindwa kurudi, aende Muhimbili anaweza kumtambua ndugu yake," alisema.

Akisimulia namna watuhumiwa hao wa ujambazi walivyouawa, Kamanda Mambosasa alisema walipata taarifa za siri kuhusu tukio hilo na kikosi kazi cha kupambana na ujambazi Mkoa wa Dar es Salaam kilianza ufuatiliaji.

"Majambazi hawa walikuwa kwenye gari T 956 BYA Toyota Noah rangi ya silver, walikuwa wakielekea kufanya uhalifu katika ghala la GS Group Ltd.

Alisema kikosi kazi hicho kilianza ufuatiliaji kulingana na taarifa za awali walizokuwa wamezipata ndipo ghafla watuhumiwa hao wa ujambazi walipoona wanafuatiliwa na wapelelezi wa kanda, waliongeza mwendo wa gari kukimbia.

"Gari la polisi liliwakimbiza na lilipowakaribia waliteremka kwenye gari walilokuwa wamepanda wakiwa wamejihami kwa silaha za jadi, lakini walianza kufyatua risasi kutoka kwenye silaha waliyokuwa nayo.

"Ndipo vijana hawa wa kikosi cha kupambana na majambazi Kanda walipojibu mapigo na kuwajeruhi majambazi hao saba kwa risasi.

"Walikamatwa na katika upekuzi walikutwa na mitungi miwili ya gesi ilikuwa ni kwa ajili ya kuwasaidia kuvunja maghala hayo, mapanga, kamba pamoja na simu."

Alisema baada ya kupekuliwa, mmoja alikutwa na silaha hiyo ya beretta ikiwa na risasi tatu ndani ya magazine ambazo zilibaki baada ya kuwafyatulia polisi.

"Majambazi wote saba walichukuliwa kupelekwa Hospitali ya Muhimbili, wakiwa wanaendelea kuvuja damu na daktari wa zamu alipowachunguza alithibitisha wote walikuwa wamefariki dunia kutokana na majeraha ya risasi walizotandikwa eneo la tukio," alisema.

Kamanda Mambosasa alisema Ijumaa iliyopita, alitoa onyo kwa watu wanaotaka kuendelea kufanya vitendo vya uhalifu Dar es Salaam, kuwa hawana nafasi na wasijutie yatakayowakuta.

"Wapo ambao wanasema sikio la kufa halisikii dawa, wamekuwa wakiendelea kujaribu kufanya vitendo vya kihalifu na unyang'anyi wa kutumia silaha. Niwaombe leo (jana) ni Idd Pili, tunaruhusu watu waendelee kufanya shughuli za kujiletea maendeleo," alisema.

Mambosasa alisema Mkoa wa Dar es Salaam umeshatoa msimamo wa shughuli ziendelee kama kawaida baada ya janga la corona lililokumba dunia kupungua.

"Kila mmoja aishi kwa kuheshimu sheria za nchi yoyote anayefanya tofauti na hapo basi atakutana nasi. Hali ya Dar es Salaam ipo shwari Sikukuu ya Idd inaendelea vizuri maeneo ya fukwe ruksa kwenda ila kila mmoja azingatie maelekezo ya Wizara ya Afya," alisema.

Pia, aliwapongeza wote wanaotoa taarifa za uhalifu ambazo zinatoa wepesi kwa Jeshi la Polisi kuwafikia watuhumiwa kabla hawajaleta madhara.

"Kuchelewa kwa majambazi hawa wangeweza kuleta madhara makubwa na wiki ya juzi tu, mama mmoja ameshambuliwa na wahuni hawa wasio na huruma kwa kupigwa risasi maeneo ya Tegeta.

HABARI KITAIFA




Mwanaharakati, Mtaalamu wa Maendeleo ya Jamii na Mwanasiasa, Dk. Mayrose Kavura Majinge akizungumza na waandishi wa habari, jijini Mwanza jana, wakati akitangaza nia yake ya kugombea urais katika uchaguzi mkuu ujao kupitia tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema). **PICHA: ROSE JACOB**

# ACT yaijibu CCM ubunge wa Zitto

**Na Enock Charles**

HATIMAYE Chama cha ACT-Wazalendo, kimeijibu hoja ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humprey Polepole, kwamba Zitto Kabwe hatarejea bungeni baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Mara kadhaa Polepole amenukuliwa akitoa kauli ya kumtaka Kiongozi Mkuu huyo wa ACT-Wazalendo (Zitto) atafute kazi nyingine ya kufanya kwa kuwa ana uhakika hatashinda kiti cha ubunge katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Zitto (43), kwa sasa ni Mbunge wa Kigoma Mjini (ACT-Wazalendo) na kabla ya hapo, alikuwa Mbunge wa Kigoma Kusini (Chadema). Mwanasiasa huyo pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).

Wiki iliyopita, Nipashe ilipata nafasi ya kuzungumza kwa faragha jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, ambaye pamoja na mambo mengine, alijibu hoja hiyo ya Polepole.

Shaibu alimkumbusha Polepole kuwa kuna tatizo la uhaba wa ajira nchini ambalo ni silaha tosha kwa ACT-Wazalendo na vyama vingine vya upinzani kuitumia wakati wa kampeni kuiharibia kura CCM.

Kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo pia alikumbusha kilio cha watumishi wa umma kuhusu kutopandishwa madaraja na kupewa nyongeza ya mishahara.

Ifuatayo ni sehemu ya mazungumzo ya Nipashe na kiongozi huyo wa ACT-Wazalendo:

**SWALI:** Kwa hali ilivyo sasa kisiasa nchi, ACT-Wazalendo ina matumaini ya kuwa na uwakilishi bungeni na hata kushinda nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu?

**SHAIBU:** Kwanza vyama vya upinzani vinao wajibu wa kufikisha ujumbe mahususi kwa umma kwamba mchakato wa uchaguzi hauna maana ni mchakato wa madaraka pekee; kwamba tunachagua wabunge, madiwani, wawakilishi pamoja na Rais. Una maana kubwa pia katika maisha yao.

Hili ndiyo tunalopaswa kulifikisha, kwamba kwa wafanyakazi wa Tanzania ambao hawajapata nyongeza ya mishahara kwa miaka mitano yote ya serikali hii, wafahamu kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya mchakato wa uchaguzi na hali inayowakumba kwa wafanyabiashara ndogondogo na wawekezaji wakubwa ambao biashara zao zimeathirika kutokana na vyuma kukaza.

Wafahamu uhusiano wa moja kwa moja yaliyokuwapo baina ya ufanisi wa biashara zao na uchaguzi wa mwaka 2020, kwa vijana kukosa ajira, vijana wa vyuo vikuu waliokosa mikopo, waandishi wa habari ambao haki zao zimebinywa.

Kwa kila Mtanzania ambaye anaona hali ya maisha imebadilika, auone uchaguzi huu kuwa una maana kubwa katika maisha yake. Kwa hiyo, hii ndiyo kazi kubwa tunayokwenda kufanya kuwavutia wananchi waweze kushiriki katika uchaguzi.

Iwapo wananchi wanautazama uchaguzi huu kama tu uchaguzi wa kuchagua mbunge, diwani na Rais, basi eeeh hawatokuja, lakini wananchi somo likiwaingia kuwa huu ni uchaguzi wao unaohusu maisha yao, unaohusu mustakabali wao, tuna uhakika kwamba wataweza kuisusia CCM.

SWALI: Mara kadhaa umeshamsikia Polepole akitamka wazi kuwa Zitto hatarejea bungeni? Hili unalizungumziaje?

**SHAIBU:** Linapokuja suala kwamba kuna ubabe unaotumika kuhakikisha CCM inashinda, kwa uzoefu tulioupata kutoka katika uchaguzi wa marudio na uchaguzi wa serikali za mitaa, kazi ya upinzani ni 'ku-mobilize' umma.

Ukiona maovu yanafanyika, umma hauchukui hatua maana yake upinzani, wanaharakati na mawakala wengine wa mabadiliko hawajauhamasisha umma vya kutosha, ili uweze kuchukua hatua.

Lakini sisi si wajinga ya kwamba kilichotokea kwenye uchaguzi wa marudio kimetokea, kilichotokea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kimetokea, basi tutakwenda uchaguzi mkuu hivyo hivyo.

Ipo kazi kubwa inaendelea kufanywa na itaendelea kufanywa wakati wa kampeni kuhakikisha kwamba yaliyojitokeza nyuma hayajitokezi tena.

Hatuwezi kutaja tunajipanga vipi kimkakati, lakini kazi kubwa inaendelea kufanywa kuhakikisha kwamba basi umma unashinda katika uchaguzi mkuu huu wa 2020.

# Wakurugenzi halmashauri kuwekwa kikaangoni

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

BUNGE la 11 linatarajia kuendelea leo, ambapo pamoja na mambo mengine, wakurugenzi wa halmashauri waliotajwa kufuja fedha katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), wanatarajiwa kujadiliwa wiki hii.

Kwa mujibu wa ratiba ya Bunge, leo wabunge wataendelea kuchangia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu taarifa za ukaguzi za CAG kwa hesabu zilizokaguliwa za serikali na mashirika ya umma kwa mwaka 2018/19.

Kesho, Bunge litaanza kujadili ripoti kuu ya mamlaka ya serikali za mitaa, iliyowasilishwa na CAG, baada ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), kuwasilisha taarifa za mkaguzi huyo, ikifuatiwa na wabunge kuijadili ripoti hiyo, serikali kujibu hoja za kamati pamoja na wenyeviti kuhitimisha siku hiyo hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti ya CAG 2018/19 iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), ilibaini viashiria vya ubadhirifu wa Sh. bilioni 1.247 uliofanywa na halmashauri 12.

Kwenye ripoti hiyo, CAG alieleza kuwa: "Serikali Kuu inapaswa kuchukua hatua dhidi ya halmashauri hizo. Uwapo wa udanganyifu huu ni ishara kuwa mamlaka za serikali za mitaa husika zinakosa utaratibu sahihi wa kubaini udanganyifu kabla haujatokea kwa kutokuwa na mifumo ya udhibiti wa ndani inayofanya kazi ipasavyo."

Vilevile, katika ripoti hiyo CAG alieleza kuwa kati ya hesabu za mwisho za halmashauri 185 zilizokaguliwa, halmashauri 176 (asilimia 95) zilipata hati inayoridhisha, halmashauri 9 (asilimia 5) zilipata hati yenye shaka.

Alieleza kuwa ingawa baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepata hati inayoridhisha, mamlaka hizo zilibainika kuwa na upungufu kutokana na kushindwa kufuata maagizo ya Bunge, sheria, kanuni, sera za serikali, na miongozo mbalimbali.

Aidha, CAG alibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 74 zilifanya manunuzi ambayo hayakushindanisha wazabuni yenye thamani ya Sh. bilioni 32.461, bila kuwa na sababu zilizojitosheleza.

Pia, alibaini kuwa mamlaka za serikali za mitaa 47 zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 9.234 ambayo hayakupitishwa na bodi za zabuni, Mamlaka za Serikali za Mitaa 34 zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni 4.353 kutoka kwa wazabuni ambao hawakuidhinishwa.

Vilevile, CAG alieleza kuwa mamlaka za serikali za mitaa 39 zilifanya manunuzi yenye kiasi cha Sh. bilioni 1.476 kwa kutumia masurufu, Mamlaka za Serikali za Mitaa 43 zilinunua na kupokea bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni tano bila kukaguliwa na kamati za ukaguzi na upokeaji wa bidhaa.

# Kesi mbunge, 'house boy' yaanza kunguruma kortini

**Na Allan Isack, ARUSHA**

KESI ya wizi iliyofunguliwa na Mbunge wa zamani wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), Anjellah Kizigha, dhidi ya mfanyakazi wake wa ndani, William Mlewa, akimtuhumu kumwibia Sh. milioni saba, imeanza kusikilizwa katika Mahakama ya Mwanzo ya Maromboso jijini Arusha.

Mashahidi watatu kati ya wanne wa upande wa mashitaka katika kesi hiyo, wamedai mahakamani kuwa hawakumwona mtuhumiwa William Mlewa akiiba kiasi hicho cha fedha nyumbani kwa mlalamikaji.

Katika kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Neema Mchomvu, mashahidi hao kwa nyakati tofauti walidai mahakamani huko, kuwa hawakumwona mshitakiwa ambaye ni kijana wa kazi nyumbani kwa mlalamikaji akiiba fedha hizo, zaidi ya kumsikia akimwomba msamaha mlalamikaji kwamba alichukua fedha hizo.

Mbele ya Hakimu Mchomvu, mlalamikaji alidai kuwa kwa mara ya kwanza Februari, mwaka huu, kulitokea wizi wa fedha nyumbani kwake na walikuwa wakiishi watu watatu akiwamo mlalamikaji, Frank Gerald na William Mlewa.

"Mara ya kwanza zilipotea fedha Sh. milioni 1.7 na baadaye zikapotea Sh. milioni mbili na mara ya mwisho wiki mbili zilizopita, zilipotea fedha zilizokuwa kwenye mfuko niliokuwa nimeuhifadhi stoo na ndani, hakuna mtu aliyejua nilipohifadhi fedha tofauti na William, lakini nilipomuuliza alikataa," alidai.

Aliendelea kudai kuwa baadaye alikwenda kuangalia tena stoo na kuukuta mfuko wa fedha na alipoufungua, ndipo alipogundua kuwa kuna kiasi cha fedha hizo zimechomolewa.

"Niliamua kuchukua kiasi kilichobaki na kuweka katika bahasha tatu na nilikwenda kanisani kutoa sadaka na baadaye nilitoa taarifa polisi," alidai.

Shahidi wa kwanza katika shauri hilo, Daniel Siuchi, alidai mahakamani kuwa alikwenda nyumbani kwa Kizigha kufanya kazi na ndani ya nyumba hiyo, alimsikia mtuhumiwa akimwomba msamaha mlalamikaji kwamba alizichukua Sh. milioni tatu na kuzitumia kwa mambo yake.

Hata hivyo, shahidi huyo alipoulizwa na hakimu kama alimwona mtuhumiwa akiiba fedha hizo, shahidi huyo alidai hakumwona.

Akihojiwa na wazee wa baraza hilo, shahidi mwingine, Tizo Yahaya (25), ambaye ni mtunza bustani, pia alidai hakumwona mtuhumiwa akiiba fedha hizo, lakini alimsikia mlalamikaji akidai kwamba fedha zake zimekuwa zikipotea mara kwa mara katika miezi Machi na Aprili mwaka huu.

Shahidi mwingine, Frank Gerald (45), ambaye alikwenda kuchomelea vyuma nyumbani kwa mlalamikaji, alidai mahakama huko kuwa mlalamikaji aliwanyima chakula kwa muda wa wiki nzima ili waseme ni nani aliyeiba fedha hizo.

Gerald pia alidai kuwa hakumwona mtu yeyote akiiba fedha hizo na kwamba mlalamikaji alifikia hatua ya kuvua nguo zake ili kuwalaani watu wote walioiba fedha hizo, huku akichukua fedha zilizopatikana kwenye begi la mtuhumiwa na kuziweka kwenye bahasha tatu na kuahidi kuzipeleka kanisani kama sadaka, ili Mungu amwonyeshe aliyeiba fedha zake.

"Mama alipotoka kanisani alirejea nyumbani na kutuuliza kwa mara nyingine ni nani ameiba fedha zake, lakini tulikana wote, ghafla William alimfuata chumbani akamwambia 'Mama ninaomba unisamehe, mimi ndiye niliyechukua fedha'," alidai.

Katika kesi hiyo, Hakimu Mchomvu aliwazuia mlalamikaji na shahidi wake,Tizo Yahya, kuzungumzia tukio la kuungua kwa uji kwa mtuhumiwa katika maelezo yao na kuwataka wajikite katika kesi ya msingi ya wizi wa fedha hizo.

Baada ya kumaliza kutolewa ushahidi huo, Hakimu Mchomvu alihahirisha kesi hiyo hadi Juni 5 mwaka huu, itakapoendelea kusikiliza ushahidi wa mwisho upande wa mashitaka.




Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeiry (wa pili kushoto), akipokea msaada wa chakula tani tano, kutoka kwa Mkurugenzi wa An-Nahl, Musa Nyamsingwa kwa niaba ya Taasisi ya Nama na washirika wake An-Nahl na Nice, jijini Dar es Salaam jana, waliojitolea kuisaidia serikali na jamii za watu wasiojiweza wakati huu wa janga la corona. Kushoto ni Mwenyekiti wa An-Nahl, Alli Kilima. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Mashirika 8 ndege za nje kuanza safari nchini

**Na Romana Mallya**

MASHIRIKA manane ya ndege yametangaza kurejesha safari zao za ndege za kuingia na kutoka mipaka ya Tanzania kuanzia Jumatatu ijayo.

Baadhi ya mashirika hayo yametangaza ndege zake kuanza safari zake Julai mosi kwa kutua Dar es Salaam, KIA, mkoani Kilimanjaro na Zanzibar.

Kwa mujibu wa tovuti ya Rick shaw travel group, inayojishughulisha na usafirishaji watalii kwenda kwenye vivutio mbalimbali kwa takribani miaka 32, safari hizo zitakuwa kwa nchi za Afrika Mashariki na kuishia kwenye viwanja vya ndege nchini.

Juni mosi, Shirika la Ndege la Tanzania linatarajia kurejesha safari zake za kuelekea Entebbe, nchini Uganda na siku inayofuata itakwenda Hahaya, Harare na Lusaka nchini Zambia.

Juni 3, safari zitakuwa Dar es Salaam kuelekea Mumbai, nchini India na Julai 2, itaelekea Bunjumbura, nchini Burundi.

Kwa upande wa Shirika la Ndege la Emirates linatarajia kuanzia Julai 2, kutokea Dubai.

Shirika la Ndege la Ethiopian Airlines, kutoka Addis Ababa, litaanza tena Juni mosi safari za ndege za kila siku kwenda Dar es Salaam, KIA na Zanzibar.

Nalo Shirika la Ndege la Kenya Airways lina mpango wa kuanza tena kutoa huduma zake nchini Tanzania kuanzia Julai 10 na zitatua katika viwanja vya ndege vya Kilimanjaro, Dar es Salaam na Zanzibar.

Shirika la Ndege la KLM, linatarajia kuanza safari zake Julai 4, kutoka Amsterdam kuelekea Kilimanjaro, Dar es Salaam.

"Shirika la Ndege la Qatar Airways lina mpango wa kuwa na ruti moja kwa siku ya usafiri kuanzia Julai 15, kati ya Dar es Salaam na Doha. Usafiri wa kuelekea Kilimanjaro hautakuwapo hadi Agosti 31, kilisema chanzo hicho.

Shirika la Ndege la Swiss litaanza safari zake kuanzia Julai mosi kupitia Nairobi kwenda Dar es Salaam na ndege hizo zitakuwa zikitokea Zurich.

Kwa upande wa Turkish Airlines, litarudisha safari zake zote za usafiri wa ndege kama kawaida kuanzia Juni 28 kama hali itakuwa nzuri.

Mashirika mengine ya ndege, Rwanda, Afrika Kusini na mengineyo hadi sasa hayajatoa taarifa zao na wengi wameonyesha kuahirisha hadi Mei 31.

## Programu yaja kuwezesha kutambua corona kwa simu

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Utoaji Huduma za Afya Aga Khan (AKHS) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aga Khan (AKU), wamezindua programu mpya kwenye simu itakayosaidia watu kutambua kirahisi dalili za corona wakiwa nyumbani na hatua za kufuata.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Aga Khan, Sisawo Konteh, katika taarifa yake jana, alisema programu hiyo ijulikanayo kama 'CoronaCheck' itaweza kupakuliwa bure kupitia simu za android na iPhone.

"Programu hii imetengenezwa na kituo cha rasilimali za afya dijiti cha mtandao wa maendeleo wa Aga Khan katika jitihada za kuunga mkono juhudi za serikali kupunguza kuenea kwa ugonjwa wa corona," alisema.

Konteh alisema sehemu kubwa ya changamoto ya corona inabadilika kwa namna wanavyofikiria kuhusu ugonjwa huo.

"Kwa kutumia programu (App), unaweza kutambua kwa haraka dalili za ugonjwa na kutafuta msaada wa kitabibu na kupima kuondoa hofu, wasiwasi, imani potofu na unyanyapaa kupitia jukwaa la ubunifu la dijiti," alisema.

Alisema programu hiyo inatumia mazungumzo ya maingiliano, ikiendeshwa na teknolojia inayoruhusu mtumiaji kuelewa dalili zake na kutambua kama tayari ameshapata maambukizo ya corona na kutafuta msaada kwa wakati.

Pia, Konteh alisema inalenga kutambua vitu vinavyoweza kubeba virusi vya corona na kupunguza uwezekano wake kusambazwa.

"Programu hii pia inaorodhesha namba za kitaifa za usaidizi wa haraka, nambari za usaidizi zinapatikana kwa kumbukumbu rahisi.

"Kifaa hiki kimepitishwa kutoka kwa huduma za afya za Alberta na kikaboreshwa kukidhi mahitaji ya nchini kwetu kwa kuangalia mlipuko wa ugonjwa."

Alisema utaalamu wa kiteknolojia wa kukuza programu umetolewa na Kituo cha Teknolojia na ubunifu cha AKU (TISC).

Mkurugenzi, Kituo cha Teknolojia na Ubunifu cha AKU, Saleem Sayani, alisema CoronaCheck inatoa fursa ya kupunguza mzigo katika mfumo wa afya.

"Matokeo yetu ya awali yanaonyesha kuwa asilimia 19 ya watumiaji walihitaji upimaji wa haraka na msaada wa matibabu.

"Hii ilisaidia kupungua kwa idadi ya watu waliokuwa wakitembelea vituo vya afya hivyo kuhakikisha rasilimali muhimu kama vifaa vya upimaji pamoja na wakati wa wahudumu wa afya kutumika kwa wale waliokuwa na uhitaji wa lazima."

Alisema CoronaCheck inalenga pia kuondoa imani potofu na upotoshaji kwa kuhusisha video za kielimu ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya taarifa ambazo hazijathibitishwa zinazozunguka kwenye mitandao ya kijamii.

# Madiwani washinikiza walipwe mapema

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda mkoani Mara, wameitaka halmashauri hiyo iwalipe stahiki zao zote zikiwamo fedha za kustaafu mapema iwezekanavyo, kabla ya kumaliza mkataba wao wa miaka mitano wakiwa madiwani.

Waliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika katika makao makuu ya Jimbo la Mwibara mjini Kibara.

Wakiongozwa na mwenyekiti, ambaye ni Diwani wa Nansimo, Sabato Mafwimbo, walisema halmashauri hiyo iwalipe stahiki zao zote kabla ya kumaliza mkataba wao wa miezi 60 na kuvunjwa kwa mabaraza ya madiwani.

Mariam Sindano, Viti Maalumu (CCM), alisema kuwa kama stahiki zao zitachelewa kulipwa, halmashauri hiyo itawasababishia usumbufu mkubwa sana, na kwamba ili kuepukana na huo usumbufu ni vyema ikawalipa mapema kabla ya kumaliza mkataba.

Akijibu hoja hiyo Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Nico Kayange, alisema madiwani hao wasiwe na wasiwasi kwani watalipwa stahiki zao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Amosi Kusaja, alisema yeye atafuata mwongozo wa Tamisemi jinsi unavyoelekeza.




Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbato Sanga (wa tano kulia), akipokea msaada wa vyakula kwa Ofisa wa Shirika la Uturuki (TIKA), Asca Sagwa, kwa ajili ya kugawa katika kaya maskini wilayani humo, mkoani Pwani jana. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

# 'Watakaohusika mimba wanafunzi waadhibiwe'

**Na Ndalike Sonda, KAHAMA**

SERIKALI imeshauriwa kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watu watakaobainika kuhusika moja kwa moja kuwapa mimba ama kuwaozesha na kuwaoza wanafunzi kipindi hiki cha likizo ndefu ya tahadhari dhidi ya corona.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mwalimu wa Malezi na Afya kutoka Shule ya Sekondari Busanda Halmashauri ya Shinyanga mkoani Shinyanga, Maria Senge wakati akizungumza na Nipashe, na kueleza kuwa shule zikifunguliwa ni lazima wanafunzi zinawakosa baadhi ya wanafunzi watoro kwa sababu ya mimba au kuolewa, hivyo kutaka sheria zichukuliwe ili iwe fundisho.

Alisema katika kipindi hiki huenda zikawapo mimba nyingi za wanafunzi kwa kuwa muda mwingi wamejiachanganya na jamii, na kwamba sheria zichukuliwa kwa wanafunzi na wote watakaosababisha mimba hizo pamoja na wazazi kutokana na kushindwa kuwalinda watoto wao.

"Likizo hii ni ndefu, kwa vyovyote kutakuwapo na wanafunzi wenye mimba, kwa hiyo serikali itoe adhabu kali kwa watu watakaobainika wamewapa mimba... hata wazazi nao wachukuliwe hatua za kisheria kwa kushindwa kuwalinda watoto wao wakati huu."

Mwalimu Senge aliwaomba wazazi na walezi kutowatumia wanafunzi katika shughuli mbalimbali za kutafuta fedha kwa ajili ya familia, na kwamba wawatumie katika kusaidia shughuli za nyumbani kisha kuwapa muda wa kujikumbusha masomo.

Naye Ofisa Jinsia na Utetezi wa Baba, Mama na Mtoto mkoa wa Shinyanga kutoka Shirika World Vison Tanzania, Magreth Mambali, aliwakumbusha wazazi na walezi kuendelea kuwalinda wanafunzi wakati huu ambao wapo nyumbani ili kutokomeza ndoa na mimba kwa wanafunzi. Alisema katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid 19, Shirika hilo limekuwa likipita na gari kwa ajili ya kutoa matangazo ya kujinga, lakini pia kutoa elimu ya kuwalinda wanafunzi wasije kujiingiza kwenye vishawishi, ambavyo vinaweza kusababisha kukatisha masomo yao.

Mratibu wa mradi wa ENRICH Tanzania unaotekelezwa na Shirika la World Vision, Dk. Frank Mtimbwa, alisema wamekuwa wakishirikiana na serikali kupitia Halmashauri na Jeshi la Polisi kitengo cha dawati la jinsia na watoto ili kuwapatika vijana elimu ya afya ya uzazi na malezi kwa vijana.

# Taasisi yasaidia makundi 5,000

**Na Futuna Selemani**

WADAU wa masuala ya maendeleo na ya kijamii nchini wametakiwa kusaidia watu wenye mahitaji maalum katika kipindi cha mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona.

Wakizungumza baada ya kupokea misaada mbalimbali kutoka taasisi ya Dorice Mollel inayosaidia watoto waliozaliwa kabla ya muda wao kwa kushirikiana na Taasisi inayosaidia jamii ya TAKI ya Uturuki kwa nyakato tofauti walisema jamii haipaswi kuwasahau.

Mwema Ramadhan, mkazi wa Bagamoyo, alisema wanaishukuru Taasisi ya Dorice kuwasaidia katika kipindi hiki kigumu duniani kutokana na janga la corona.

"Tunaomba na wadau wengine wajitokeze kutusaidia sisi wenyewe maisha magumu, Mwenyezi Mungu atawalipia", alisema Mwema.

Ramadham Salum alishukuru DORICE na TAKi kuwasaidia, na kuomba wasiishie hapo kwani wapo wengi wanaohitaji misaada kama hiyo hasa kwa kipindi hiki.

Kwa upande wake Mwanzilishi wa Taasisi ya DORICE Mollel inayosaidia watoto waliozaliwa kabla ya Sikh zao, alisema walianza kusaidia kaya 400 miaka mitatu iliyopita, lakini sasa wamefika ZAIDI ya elfu tano katika baadhi ya wilaya mkoani Pwani na jijini Dar es Salaam.

Alisema pia wamekuwa wakisaidia baadhi ya hospitali kwa kutoa vifaa mbalimbali kwenye wodi za watoto njiti kama dhamira Take alivyokusudia kwani yeye ni mmoja wa watoto wa kundi hili.

"Tutaendelea kusaidia jamii ya makundi maalum wenye mahitaji bila kubagua na mwaka huu tumesaidia futari vyakula kwa ajili ya sikukuu... utaratibu huu tutaendelea nao, hautakwama kadri itakavyokuwa," alisema Dorice.

Kwa upande wake Ofisa Programu wa Taasisi ya TAKI ya UTuruki inayosaidia jamii, Badru Yassin, alisema.kuwa Taasisi hiyo inasaidia jamii serikali ma Taasisi zisizo za kiserikali katika kupambana na umaskini.

"Tunawafikia walengwa hadi majumbani taasisi zimazohitaji misaada lwa lengo la kusaidia wananchi tunafanya nao kazi pamoja hatubagui lengo ni kusaidia jamii," alisema

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunazingatia kuwapa mabinti ulinzi zaidi

KATIBA ya Tanzania ya mwaka 1977 inaeleza kuwa Watanzania wote wamezaliwa huru na wako sawa mbele ya sheria na kwamba bila kubaguliwa, kila mmoja anastahili kutambuliwa utu wake, ni kwa mujibu wa Ibara ya 12 (1).

Kadhalika inaendelea kuwahakikishia wanawake, watoto, wanaume, wazee wenye ulemavu na raia wote kuwa wako huru mbele ya sheria na wanastahili kulindwa bila ya yeyote miongoni mwao kutendewa kinyume cha sheria.

Aidha, kuna mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania imeiridhia inayozitaka nchi wanachama kutunga sheria ambazo zinawalinda raia wote wakiwamo watoto.

Aidha, Malengo Endelevu ya Mileniam ya Umoja wa Mataifa (lengo 5.3) linawataka wanachama wa umoja huo kutokomeza mila potofu, zinazochangia ukandamizaji watoto kabla ya 2030.

Aidha, Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki za Binadamu Itifaki ya Haki za Wanawake unasema wanaume na wanawake wanapaswa kuwa washirika sawa katika ndoa na pande zote lazima zitoe ridhaa ambayo inaweza kutolewa na watu wazima wenye zaidi ya miaka 18.

Yote haya ni mambo yanayoichochea Tanzania kukomesha mimba kwa watoto kwa kuwa na sheria na sera zinazowalinda mabinti wasiolewe katika umri mdogo, wala kupata mimba utotoni au kukwamishwa kwa namna yoyote na masuala yanayohusu ngono na ubakaji watoto.

Tunasema haya kwa sababu watoto wako likizo na ya zaidi ya miezi miwili sasa ili kujihadhari na corona na mara nyingi wadau wa utetezi wa watoto wamekuwa wakionya kuhusu mabinti kutumbukia katika janga la mimba za utotoni.

Wastani wa hali ya mimba za utotoni nchini mwaka 2017 ilikuwa ni asilimia 27. Ikionyesha kuwa ni wastani wa watoto kuzaa chini ya umri wa miaka 18 ni asilimia 27. Kwa muijibu wa takwimu za mwaka 2016/17 zilizotolewa na Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS).

Ukiangalia hizo takwimu zinatisha. Pengine kwa wakati huo kwa maana kama kuna watoto 100 ambao walitakiwa shuleni pengine darasa la sita, au kidato cha pili 27 waliacha masomo kwa kuwa wamepata mimba au wameozeshwa ndoa za utotoni.

Kwa kutumia takwimu hizo huenda wakati huu wa likizo ya corona hali ikawa mbaya zaidi kwa hiyo, wakati huu serikali inapotangaza kufunguliwa upya shule kwa masomo ya kidato cha sita wazazi na walezi wazingatie sana ulinzi wa mabinti na kuchukua tahadhari.

Kwa kuangalia takwimu za NBS za mwaka 2016/17 inamaanisha kuwa kila walipo mabinti wa Tanzania wanaotakiwa pengine kuendelea na masomo ya shule za msingi au sekondari asilimia 27 inakwamishwa na ama mimba au ndoa mambo yote yakiwa ni kuendeleza unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.


Hali hiyo si ya kubeza kwani taifa linapoteza nguvu kazi kubwa kila wakati kuwasomesha, Lakini pia mabinti nao wanahatarisha maisha yao, mathalani afya zao ziko rehani kuzaa utotoni. Maendeleo yao na ndoto zao zinakatishwa kutokana na mimba hizo.

Kwa wakati huu ndiyo muda wa wadau mbalimbali kuanza kuisimamia serikali na kuona kuwa inatekeleza mpango kazi wa taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wenye ajenda kubwa ya kupunguza mimba na ndoa za utotoni.

Tunaamini kuwa hilo linawezekana kwa kuwapa wananchi elimu kwa vile changamoto vijijini ni kuwafikia wananchi na kuwahamasisha kuacha mambo yaliyopitwa na wakati hasa mila duni, potofu na kandamizi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi, walezi anzeni kubeba gharama hizi



Na Sabato Kasika

JUMATATU ijayo Juni mosi wanafunzi wa kidato cha sita na wa vyuo vikuu wanatarajia kuanza masomo baada ya serikali kujiridhisha kuwa maambukizo ya virusi vya corona yanapungua.

Kutokana na hali kuendelea vizuri, imeamua kuruhusu wanafunzi wa kidato cha sita na vyuo vikuuu kuanza masomo huku wa shule za msingi hadi kidato cha tano wakitakiwa kusubiri kwanza.

Hatua hiyo ya serikali kutangaza kufungua vyuo, mamlaka zinazohusika na masuala ya taalamu zitawajibika kuandaa mpango ili kuwawezesha wanafunzi kufidia muda wa masomo walioukosa.

Pamoja na hatua hizo za kufungua vyuo, bado wazazi wana wajibu wa kuhakikisha watoto wao wanaendelea kuwa salama, wawapo kwenye masomo, wakati huu ambao maambukizo ya corona yanaendelea kupungua.

Tayari, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi) anayeshughulikia Elimu, Mwita Waitara ameshaagiza viongozi wa mikoa, wilaya na uongozi wa shule za kidato cha sita kuchukua tahadhari zote za afya ikiwamo wanafunzi wa bweni kulala kwa umbali ili kujiepusha na maambukizo ya ugonjwa wa corona na kukagua mazingira ili yasiwe sababu ya maradhi.

Tahadhari nyingine ambayo inasisitizwa ni kuhakikisha wanafunzi wote na walimu wao wanavaa barakoa na kunawa mikono kwa maji tiririka kwenye maeneo yote ya kuingilia shuleni na madarasani.

Katika hilo, anaeleza kuwa kuna uwezekano wazazi wakaingia gharama kidogo, kwa vile wanatakiwa kuwanunulia watoto wao barakoa na pia vitakasa mikono ili kujikinga na ugonjwa huo.

Kwa upande wa walimu, wanatakiwa kuwaandaa wanafunzi kisaikolojia ili wafanye vizuri kwenye mitihani yao ingawa pia wanafunzi wanaweza kwenda na tangawizi ili kujifukiza, lakini pia ni lazima wapimwe joto.

Maelekezo hayo yanagusa pande zote, hivyo ni muhimu zihusika kwa ajili ya usalama wa wanafunzi, wanaotarajiwa kuanza masomo mwezi ujao ili waweze kusoma bila changamoto ya maambukizo ya corona.

Wazazi wasiwe wazito katika kuchangaia usalama wa afya za watoto wao kwa kukwepa gharama za kuwanunulia barakoa na vitakasa mikono wakitegemea kwamba watafanyiwa kila kitu.

Serikali imeshaweka wazi kwamba katika hilo, kuna uwezekano wazazi kuingia gharama kidogo, hivyo walipokee hilo na kuanza kulifanyia kazi, kwani uhai una gharama kubwa kuliko fedha.

Jambo jingine la msingi ni wanafunzi wenyewe kutambua na kuzingatia kwamba ugonjwa huo upo, hivyo suala la kuchukua tahadhari ni la msingi kwa ajili ya usalama wa afya zao.

Kwa kawaida penye wengi huwa kuna mengi na pia kuna walimu wengi wakiwamo wa kupotosha, ambao wanaweza kusababisha baadhi ya wanafunzi wakaacha kuzingatia maelekezo wakidhani wako salama.

Yawezekana ukafika wakati wakaacha kuvaa barakoa au kunawa kwa maji tiririka na pia kupata vitakasa mikono kwa kufuata elimu za vijiweni hali ambayo inaweza kusababisha wakajikuta katika matatizo.

Hivyo suala la umakini ni la muhimu kwenye vita dhidi ya corona, kwani ndiyo umekuwa msisitiza serikali, kwamba corona imeanza kupungua, lakini ni vyema Watanzania kuchukua tahadhari.

Ni vyema kuzingatia kwa sababu imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya watu mitaani kupingana na maelekezo ya wataalamu wa afya kuhusu kujikinga na ugonjwa huo na kwamba wao ndiyo wanajua zaidi.

Hayo yanaweza kuingia hata shuleni na kusababisha wanafunzi wasiwe makini wakidhani si lazima kunawa kwa vitasaka mikono au kunawa kwa maji tiririka na kumbe wanapotoshwa.

Lakini, kikubwa zaidi ni kwamba wazazi wafanye sehemu yao kwa kuingia gharama ya kuwanunulia watoto wao barakoa na vitakasa mikono ili wakavitumie mara shule zitakapofunguliwa.

Suala la kuingia gharama kidogo kwa ajili ya usalama wa afya za watoto halikwepeki, cha msingi ni kuliwekea mikakati ili kulifanikisha kwani zinahitajika barakoa za kutosha na vitakasa mikono vingi.

# Tanzania ilivyopata kwa tabu mkopo AfDB ujenzi U/ndege

**Novatus Makunga, ARUSHA**

MKURUGENZI Mtendaji mstaafu wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Dk. Nyamajeje Weggoro, ameeleza jinsi mchakato wa kupata fedha za ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato wa mjini Dodoma kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 757.7 ulivyokuwa mgumu.

Dk. Weggoro ambaye alistaafu kama mkurugenzi mtendaji wa benki hiyo yenye makao makuu yake mjini Abidjan Ivory Coast Aprili mwaka jana, alielezea mchakato huo katika mahojiano yake na kituo kimoja cha runinga jijini mjini hapa jana.

"Miongoni mwa mafanikio yaliyonipa faraja nikiwa AfDB ni kwa nchi kupata mkopo huo wa masharti nafuu kwa ajili ya kutekeleza mradi muhimu wa kujenga uwanja kwenye mji ambao ni makao makuu ya serikali," alisema.

Dk. Weggoro ambaye kabla alikuwa msaidi wa Rais wa masuala ya uchumi, alisema ilikuwa vigumu kwa benki hiyo kutoa fedha za uwanja huo kwa kuwa mjini wa Dodoma upo katikati ya nchi kwa hiyo hawakuona umuhimu wa kuwa na uwanja mkubwa wa kimataifa.

Alisema alilazimika kuwaleta wakurugenzi wa bodi wa benki hiyo ambao walitembelea Dodoma na pia kukutana na viongozi mbalimbali wa serikali waliotoa maelezo ya kina ambayo yaliwezesha kupatikana kwa fedha za ujenzi.

Alisema benki hiyo ilitoa dola za Marekani milioni 272.2 (sawa na shilingi bilioni 757.78), huku serikali ikichangia asilimia 17 ya fedha hizo ambazo ni sawa na shilingi bilioni 133.03.

Mchakato wa zabuni ya ujenzi wa uwanja huo utakaokuwa na barabara ya ndege yenye urefu wa kilometa 3.6, majengo ya kisasa ya kuhudumia abiria ulifungwa rasmi Aprili 19, mwaka huu.

"Uwanja utarahisisha kuunganisha nchi na maeneo mengine duniani na ilikuwa faraja kwa bodi ya wakurugezi kuidhinisha fedha hizo na sasa utauweka mji wa Dodoma katika anga za kimataifa," alifafanua.

Aidha, Dk. Weggoro alitaja miradi mwingine wa majisafi na majitaka wa Jiji la Arusha uliopata mkopo nafuu wa shilingi bilioni 520 pamoja na wa barabara za mchepuko za mji huo.

Kwa mujibu wa Dk. Weggoro, benki hiyo pia ilitoa fedha za kukamilisha kipande kilichobaki kati ya Dodoma na Babati kipitia Kondoa cha kilometa 210 zilizobaki za barabara kuu ya Afrika inayotokea kusini katika mji wa Capetown, Afrika Kusini hadi kaskazini mwa mji wa Cairo nchini Misri yenye urefu wa kilometa zaidi ya 10,000.

Alisema AfDB katika kipindi chake iliidhini mkopo wa Euro milioni 345 kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara inayoambaa na Pwani ya Bahari ya Hindi ya kutoka Mombasa-Lunga Lunga na Hororo nchini Kenya mpaka Tanga-Pangani hadi Bagamoyo.

"Barabara hii itasaidia kukuza utalii wa nchi za Afrika ambapo katika Mto Pangani patajengwa daraja kubwa, hivyo kuondoa adha ya sasa ya kutumia kivuko," aliongeza.

Hata hivyo, Dk. Weggoro alisema bado kuna tatizo kubwa la watu na taasisi binafsi kukopa katika benki hiyo ukilinganisha na nchi nyingine ikiwamo Kenya.

Alisema hali hiyo inatokana na idadi kubwa ya Watanzania kutokuielewa benki hiyo, ambapo alisema mikopo yake ina masharti nafuu sana ikiwamo ya miradi ya elimu na biashara.

Benki hiyo ilianzishwa mwaka 1964 mjini Logos, Nigeria na nchi 23 ambapo Tanzania ilijiunga mwaka 1971 ikiwa na wanahisa ambao ni nchi 81 zikiwamo 54 zote za Afrika.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, akijibu hoja mbalimbali wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, mkoani Singida mwishoni mwa wiki. **PICHA: ELISANTE JOHN**

# Mufti aitaka jamii kusaidia wahitaji

**Na Mary Geofrey**

MUFTI wa Tanzania, Abubakar Zuber, amewataka Watanzania wenye uwezo kujitoa kusaidia jamii zenye uhitaji hasa walioathirika na janga la corona.

Wito huo aliutoa jana jijini Dar es Salaam, wakati akipokea misaada ya chakula kwa ajili ya kusaidia kaya 100 zenye uhitaji zilizo chini ya Baraza Kuu la Waislam Tanzania (Bakwata), kutoka taasisi ya Nama kupitia washirika wake, Annahl Trust na Nice Tanzania.

Alisema ni muhimu jamii za watu wenye uwezo kusaidia wasio na uwezo bila kubagua dini, rangi wala kabila na kwamba misaada waliyopokea kwa niaba ya wahitaji itawafikia kikamilifu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Annahl Trust, Mussa Nyamsingwa, alisema wamemkabidhi Mufti misaada ya chakula kwa ajili ya watu wasiojiweza, wenye ulemavu, yatima na wajane waliopo Bakwata kwa ajili ya kuwasaidia kujikimu wakati huu wa janga la corona.

Alisema wamemkabidhi misaada hiyo ambayo kila kaya itapata unga kilo 10, mchele kilo 10, maharagwe, mafuta, sabuni, barakoa na vitakasa mikono kwa ajili ya kujikinga na familia zao.

Alisema hiyo ni sehemu ya misaada ambayo wanatarajia kutoa kwa kaya 5,000 katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Visiwani Zanzibar yenye thamani ya Sh. milioni 800.

Alieleza kuwa wamelenga kutoa misaada ya Sh. bilioni 1.3 ikiwa ni pamoja na vifaa tiba watakavyokabidhi kwa serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, vitakavyogaiwa katika hospitali mbalimbali nchini.

Mwisho

# Madiwani walia na zao pamba

**Na Ahmed Makongo, BUNDA**

MADIWANI katika Halmashauri ya Mji wa Bunda mkoani Mara, wameonyesha wasiwasi mkubwa juu ya mwelekeo wa zao la pamba katika msimu ujao.

Wamedai kuwa wakulima wa pamba wilayani hapa wamepoteza matumaini kutokana na uzalishaji wa zao hilo kutoleta tija kwao.

Waliyasema hayo wakati wakichangia hoja hiyo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha Baraza la Madiwani mjini Bunda.

Walieleza baadhi ya sababu zinazofanya zao hilo kukosa tija na kusababisha wakulima kukosa matumaini kuwa ni pamoja na ukosefu wa viuatilifu.

Aidha, walisema kuwa hata viuatilifu hivyo vinapopatikana vimekuwa vikiuzwa kwa bei kubwa, ambapo chupa moja imekuwa ikiuzwa kwa bei ya Sh. 37,000, ambapo walidai ni ya juu mno.

"Wakulima wengi wamekosa matumaini na zao la pamba kutokana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo ikiwamo ya ukosefu wa viuatilifu vyenye ubora," alisema mmoja wa madiwani hao.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bunda, Abraham Mayaya, aliliambia baraza hilo kuwa licha ya viuatilifu (dawa) hivyo kuuzwa kwa bei ya juu, lakini haijasaidia kuua wadudu mashambani badala yake mashamba mengi ya wakulima hao hayajatoa mazao bora.

Mayaya alisema kutokana na hali hiyo, huenda wakulima hao wakakosa kabisa mavuno, jambo ambalo alisema ni hatari kwani hawataweza kurejesha mikopo ya pembejeo waliyokopa kutoka kwa wafanyabiashara nchini, baada ya Bodi ya Pamba kujitoa kuwa mdhamini wa wakulima katika msimu wa mwaka huu.

**"Wakulima wengi wamekosa matumaini na zao la pamba kutokana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo ikiwamo ya ukosefu wa viuatilifu vyenye ubora," alisema mmoja wa madiwani hao.**

# Wawekezaji waahidiwa kutatuliwa changamoto

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki, amewatoa hofu wawekezaji na wafanyabiashara juu ya changamoto mbalimbali zinazowakabili na kuahidi kwamba serikali ipo katika mchakato wa kuanzisha sheria mpya ya uwekezaji.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, Kairuki alisema kuwa serikali ina mipango na mikakati ya kuhakikisha kuwa inaendelea kuimarisha mazingira bora ya uwekezaji nchini.

"Serikali inatambua changamoto wanazopitia wawekezaji na imeweka mikakati ya kuhakikisha inazitatua ikiwamo uanzishwaji wa sheria mpya ya uwekezaji nchini inayolenga kuweka mazingira bora ya uwekezaji na kutatua changamoto mbalimbali za kibiashara,"alisema Kairuki.

Miongoni mwa changamoto ambazo wawekezaji walitaja kukabiliana nazo ni pamoja na utitiri wa kodi, ukosefu wa maji ya uhakika, ubovu wa miundombinu ya barabara, gharama kubwa za uzalishaji na uzalishaji duni.

Changamoto nyingine walisema ni ugumu wa kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika, ukosefu wa utaalamu katika kilimo, pamoja na uwapo wa bidhaa zisizo na ubora sokoni.

Akijibu changamoto hizo, Waziri Kairuki alisema pamoja na serikali kufuta kodi zaidi ya 160, lakini itaendelea kuboresha miundombinu muhimu ikiwamo barabara zinazosimamiwa na Tarura na kuweka mazingira ya uhakika ya upatikanaji wa umeme .

Mchumi Mkuu wa idara ya Uwekezaji, Francis Mollay, alisema miongoni mwa jitihada wanazofanya ni pamoja na kupitia sheria na sera zinazohusiana na kodi ili kuhakikisha wawekezaji wananufaika na uwekezaji wao pamoja na uwapo wa sheria na kanuni bora zinazoweka mazingira mazuri ya kuboresha sekta hiyo.

"Tunaendelea kuboresha mazingira ya biashara kwa kupitia sheria na sera zinazohusiana na kodi mbalimbali ili kutatua changamoto za kikodi zilizopo," alieleza Mollay.



Taka za wafanyabiashara wadogo katika kituo cha daladala na bajaji cha Mbezi Mwisho, kuelekea Kinyerezi jijini Dar es Salaam, zikiwa zimerundikwa na kutelekezwa pembeni ya kituo hicho juzi, na kusababisha usumbufu kwa madereva wa bajaji na wapita njia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wengine Chadema Tarime watimkia CCM

**Na Timoth Itembe, MARA**

SIKU chache baada ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mkoa wa Mara, Mwita Joseph kukihama chama chake na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM), katibu wake naye jana amejiengua kwenye chama hicho na kujiunga na CCM.

Wengine waliohama na kujiunga na CCM ni Boniface Mwita, ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Kata ya Matongo, George Nyanchama, aliyekuwa Mwenyekiti wa kijiji cha Kyasangura, Emanuel Magige, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kata ya Nyandoto, kupitia ACT-Wazalendo na Nashoni Mchuma, ambaye alikuwa mgombea udiwani kata ya Gwitiryo kupitia Chadema, 2015.

Akiwapokea, Mwenyekiti wa CCM Wilaya Tarime, Daudi Ngicho, alisema wapinzani kwa sasa hawana nafasi Tarime na uchaguzi ujao watafute kazi ya kufanya.

Ngicho alisema CCM Tarime imeimarika kwa sababu ya utendaji kazi wa Rais John Magufuli pamoja na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Tarime, Daudi Ngicho na Naibu Waziri Tamisemi, Mwita Waitara.

Katibu wa CCM Wilaya ya Tarime, Kamisi Kura, alisema Chadema Tarime imepata pigo kukimbiwa na viongozi wa ngazi ya juu akiwamo Katibu na Mwenyekiti, na kuwa hizo ni juhudi za Rais John Mgufuli za utendaji kazi wake wa kuwaletea wananchi maendeleo na kusimamia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015-2020.

Naye Naibu Waziri Tamisemi alisema kuwa hali ya Chadema itaendelea kuwa mbaya wilayani Tarime na Tanzania kutokana na watu kuendelea kujitambua na shughuli anazozifanya Rais Magufuli.

Aliyekuwa Katibu wa Chadema Wilaya ya Tarime, Samweli Nyandula, alisema amehamia CCM kwa matakwa yake bila kulazimishwa na mtu.

# Aomba msaada matibabu ya mwanawe kwa JPM

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

MKAZI wa Kijiji cha Endakiso Kata ya Endakiso, Adam Bombo, amemwomba Rais John Magufuli kumsaidia kupata matibabu ya mtoto wake, Asha Adam (14), anayesoma darasa la sita katika Shule ya Msingi Endakiso aliyevimba bega na kuambiwa apate matibabu Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Akizungumza na Nipashe, baba wa mtoto huyo alisema mwanawe alipata ajali ya baiskeli wakati akitoka kuchukua mahitaji.

"Mtoto wangu alipoumia hakusema kwa mama yake, na mimi hakuniambia akawa anaenda shule hivyo hivyo," alisema Bombo.

Aidha, alisema mtoto huyo aliendelea na kuuami bila kusema, lakini baada ya siku nyingi kupita ndipo alimwambia mama yake kuwa anaumwa begani.

Alisema Asha alimwambia kuwa alianguka na baiskeli ila akaona ni hali ya kawaida maumivu yataisha kumbe ndio yanazidi.

Bombo alisema baada ya kubaini hali hiyo alimpeleka Hospitali ya Mji wa Babati Mrara na kupewa rufani ya kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara.

Alisema baada ya kufikishwa alihudumiwa ila akaambiwa hawana vifaa vya kumfanyia uchunguzi zaidi, na kupewa rufani ya kwenda Hospitali ya Hydom.

"Nilirudi nyumbani nikatafuta fedha Sh. 500,000 nikaenda Hospitali ya Hydom, lakini nao walisema hawana vifaa vya kuchunguza, niende Muhimbili au KCMC," alieleza.

Alimwomba Rais Magufuli na Wizara ya Afya kumsaidia mtoto wake apate matibabu kwa kuwa yeye hana uwezo, na ameambiwa matibabu yatagharimu Sh. milioni 1.5.

Alifafanua kuwa toka mtoto awe hivyo ni wiki tatu kubaini ugonjwa huo.

Mawasiliano zaidi mzazi wa mtoto ni 0683203363.

HABARI KITAIFA

# Hati safi Mafinga yamkuna RC Hapi

**Na Francis Godwin, IRINGA**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, amepongeza Halmashauri ya Mji wa Mafinga kwa kupata hati safi ya ukaguzi kwa hesabu za mwaka ulioishia Juni 30 mwaka 2019 kwa hesabu za jumla na miradi ya maji.

Miradi mingine ni mfuko wa pamoja wa afya na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ukiwa ni mwaka wa tatu mfululizo kwa halmashauri hiyo kupata hati safi.

Akizungumza juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani, alisema kuwa heshima kubwa ambayo Halmashauri ya Mji wa Mafinga imepata ni heshima ya mkoa mzima wa Iringa, na kwamba kuwa pamoja na halmashauri zote tano zimeweza kufanya vizuri na kuufanya mkoa huo kuzidi kung'ara kwa kuwa na hati safi kwa kila halmashauri.

"Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza madiwani na watendaji wote wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga chini ya mkurugenzi kwa kuiwezesha halmashauri hii kuwa na heshima ya hati safi. Pia nazipongeza halmashauri zote tano za mkoa wa Iringa kwa kupata hati safi za ukaguzi kwani kitendo hiki kimeupa heshima kubwa mkoa wetu, ila naomba mzidi kufanya vizuri zaidi."

# Corona yabadili mfungo Ramadhani

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

HOFU ya maambukizo ya virusi vya corona imetajwa kubadili baadhi ya tamaduni na miongozo ya dini ya Kiislamu.

Imeelezwa kipindi chote cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani baadhi ya waumini wa dini hiyo wamejikuta wakishindwa kufunga kutokana na hofu ya kuugua ugonjwa huo.

Akizungumzia athari zilizojitokeza wakati wa Ibada maalum ya Idd el Fitri Manispaa ya Morogoro, Mhadhiri Mkuu Msikiti wa Boma, Ally Ramadhani, alisema kuwa mfungo wa mwaka huu hautafutika katika historia, kwani hofu ya ugonjwa wa corona imebadili mwenendo wa dini hiyo.

# Wataka msisitizo matumizi sahihi maji, vitakasa mikono

**Na Shaban Njia, MBOGWE**

WADAU wa afya wilayani Mbogwe mkoani Geita wameiomba serikali kuweka msisitizo katika matumizi ya maji na vitakasa mikono kwenye maeneo yenye mikusanyiko ya watu.

Maeneo hayo ni minada na maegesho ya magari ili kujikinga na ugonjwa wa Covid-19.

Meneja Mradi wa Badilisha Tabia Epuka Covid-19 wa Shirika lisilo la Kiserikali la Shdepha+, Martin Nyakitina, aliyabainisha hayo katika hafla ya kutambulisha mradi wa kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo na kukabidhi vifaa vya kujikinga na ugonjwa huo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Matha Mkupas.

Alisema mradi huo utagharimu Sh. milioni 30 na utatekelezwa kwa miezi mitatu na unalenga kuwafikia wakazi wote wa mijini na vijijini ili kuhakikisha wanachukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

"Zoezi hili litafanyika kwa njia shirikishi ambapo sisi SHDEPHA+kwa kushirikiana na maofisa wa idara ya afya tutatembelea maeneo yenye mikusanyiko na kuwakumbusha wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya janga la corona," alisema Nyakitina.

Alisema mradi huo utahusisha elimu kwa njia ya vyombo vya habari ambapo maofisa wa afya watapata fursa ya kutoa elimu hiyo kwa wananchi ili kufikia maeneo yote ya wilaya hiyo hususani wale wa vijijini na kutoa vipeperushi vyenye ujumbe kuhusiana na corona.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbogwe, Benedict Sylivester, alisema wameanza kuwachukulia hatua za kisheria baadhi ya wananchi ambao hawazingatii maelekezo ya serikali kwa kutoweka vifaa vya kunawia mikono katika maeneo yao ya biashara.

"Kupitia sheria ndogo za halmashauri tunaendelea kuwatoza faini wafanyabiashara wanaobainika kukiuka maagizo ya serikali, lakini kupitia elimu watakayopatiwa na Shdepha+ itasaidia kuongeza msisitizo katika mapambano ya ugonjwa huo hususani katika eneo la Mji Mdogo wa Masumbwe," alisema Sylivester.

Naye DC Mkupas alisema kuwa elimu zaidi inahitajika kwa wananchi hasa wa vijiji na kuwataka kutopuuza maagizo ya wataalamu wa afya kuhusiana na suala la unawaji mikono ili kujikinga na ugonjwa wa Covid -19.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko, akizungumza na wachimbaji wadogo katika mgodi mdogo wa Mwabomba, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga jana, wakati akitatua mgogoro uliodumu zaidi ya miaka 20 kati ya wachimbaji hao na kampuni ya utafiti wa madini ya Catton Myabi Tanzania Ltd. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Ikungi yalipa wakulima mil. 120/-

**Na Elisante John, IKUNGI**

HALMASHAURI ya Ikungi, mkoani Singida imetumia zaidi ya Sh. milioini 120 kwa ajili ya ununuzi wa choroko za wakulima kwa mnada kupitia vyama vyao vya msingi.

Akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema wakulima wanaendelea kulipwa fedha zao moja kwa moja kupitia vyama vyao vya msingi, chini ya idara ya ushirika.

Alisema kuwa fedha hizo zimenunua choroko zaidi ya tani 40 zilizokusanywa baada ya kununuliwa kutoka kwa wakulima, na kwamba lengo ni kuwawezesha kuyafikia masoko na kuondokana na changamoto ya kuchelewa kuuza mazao yao.

"Kilo moja kwenye mnada wa choroko ni takribani Sh. 1,075, faida waliyopata wakulima ni ya mara mbili zaidi kuliko ile ambayo wakulima wetu walikuwa wanapewa hapo mwanzo na walanguzi wa zao hili, wanaotaka kuwanyonya wananchi wetu," alisema Kijazi.

Naye, Mkuu wa wilaya hiyo, Edward Mpogolo, alisema bei ya mnada wa zao hilo inafikia hadi Sh. 1,200, wakati ile ya walanguzi ilikuwa kati ya Sh. 400 hadi 600 kwa kilo moja.

Vile vile, alisema kwa sasa wakulima wananufaika kwa mapato makubwa, ikilinganishwa na awali ambako pamoja na kuvuja jasho jingi hawakupata soko la uhakika la mazao yao.

Baadhi ya madiwani, Halima Ng'imba, walieleza wasiwasi wao mfumo huo mpya, kwa madai kuwa unachelewesha malipo ya wakulima wakati huu ambao wengi wao hasa wa maeneo ya vijijini, wamekumbwa na mafuriko, hivyo kuhitaji fedha za haraka.

Alisema baadhi ya wakulima wanaingia kwenye mgongano na serikali, kutokana na kiasi kidogo cha choroko walichovuna, ambacho ni chini ya kilo nne, hali inayolazimu wauze kwa bei ya Sh. 400 au 600, ili angalau kupata fedha za kujikimu.

"Saccos yenyewe haina fedha, lakini mtu unamwambia akaiweke, ukiichukulia jamii yetu ya vijijini inahangaika, haina hata nyumba...halafu wewe unamwambia akaweke kwenye chama cha ushirika au sacoss, badala auze ili akanunue hata turubai akamsitiri mtoto wake," alibainisha.

Akihitimisha mjadala huo, Mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya hiyo, Ali Mwanga, alisema kuwa mfumo huo utaiwezesha serikali kupata kodi sahihi na kwa wakati, huku akibainisha mfumo huo mpya utahusu zao la choroko, ufuta, dengu na mbaazi.

Alisema mazao hayo katika Wilaya ya Ikungi yatakuwa yanauzwa kwa utaratibu wa mnada, lengo likiwa kumwepusha mkulima asipunjwe bei na walanguzi, pia halmashauri ya wilaya, serikali na vyama vya ushirika na msingi, navyo vitanufaika na mapato.

# Tarura yatakiwa kufuata vipaumbele vya h/shauri

**Na Julieth Mkireri, CHALINZE**

MBUNGE wa Jimbo la Chalinze Ridhiwani Kikwete ameushauri Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (Tarura) kutengeneza barabara kwa kufuata vipaumbele vya halmashauri na wananchi badala ya kupanga wao wenyewe maeneo ya kuyafanyia kazi.

Ridhiwani alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki kwenye Baraza la Madiwani lililofanyika Lugoba katika Halmashauri ya Chalinze Wilaya ya Bagamoyo.

Alisema, Tarura wanatakiwa kuwashirikisha madiwani ambao wanatambua barabara ambazo ni korofi zinazosababisha baadhi ya shughuli za wananchi kutofanyika kwa wakati.

"Tushirikisheni katika ukarabati wa barabara, tumesisitiza Tarura wasikae kufanyia kazi vipaumbele vyao, watushirikishe... lakini washiriki kwenye mikutano ya wananchi watatambua maeneo ambayo ni korofi ya kuyafanyia kazi," alisema Ridhiwani.

Naibu Waziri wa Nishati ambaye ni Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Pwani, Subira Mgalu, aliomba wataalamu wanapoanza michakato mbalimbali kuwashirikisha wabunge na madiwani ili wapate fursa ya kuishauri serikali.

Naye Diwani wa Kiwangwa, Malota Kwaga, aliomba Tarura kutumia vizuri fedha wanazopata kufungua barabara ambazo ni msaada kwa wananchi.

Meneja wa Tarura Halmashauri ya Chalinze, Mhandisi Henrico Shauri, alisema anakabiliana na changamoto ya ufinyu wa bajeti, pamoja na kutopata michango kutoka kwenye mapato ya ndani ya halmashauri hiyo katika utengenezaji wa barabara.

Shauri alisema, amepokea ushauri uliotolewa kutoka katika baraza hilo, na kuahidi kuzifanyia kazi wakati wa utekelezaji wa shughuli za barabara.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Zainabu Makwinya, alisema kuhusiana na kuchangia mfuko wa barabara kwa fedha za mapato ya ndani watafanya vikao kujadili suala hilo kwa kushirikiana na wataalamu wa Tarura.



Wakazi wa Manispaa ya Iringa, wakitoka kununua mbuzi kijijini kwa ajili ya kitoweo cha sikukuu ya Eid El Fitri, juzi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wapewa mamilioni elimu ya corona

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Huheso Foundation lililopo wilayani Kahama mkoani Shinyanga, limepewa kiasi cha Sh. milioni 30 na The Foundation for Civil Society(FCS) kwa ajili ya kutoa elimu ya ukatili wa kijinsi kama moja ya kupambana na ukatili unaotokana na virusi vya Covid-19.

Akitambulisha mradi wa baki salama jana Mkurugenzi wa Shirika hilo, Juma Mwesigwa, mbele ya Mganga Mkuu wa Hospitali ya wilaya, Devid Lucas, Ofisa Afya Basil na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, Anderson Msumba, alisema mradi huo utatekelezwa kwenye kata tano zilizopo halmashauri hiyo.

Alisema wamepokea fedha hizo kwa ajili ya kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa wa Covid-19 pamoja na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto kwenye kata tano, na kwamba mradi huo utatekelezwa kwa miezi mitatu.

Aidha, Mwesigwa alizitaja kata ambazo mradi unakwenda kutekelezwa ni Majengo, Nyasubi, Zongomela, Kahama Mjini na Malunga. Alisema ili kudhibiti wimbi la ukatili wa kijinsia, watatoa elimu kwa mpango wa Taifa wa kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) kata na wilaya.

"Ugonjwa wa Covid-19 bado upo licha ya kuendelea kuchukua tahadhari, fedha tulizozipata tutaelekeza kwenye kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa na kutoa elimu ya ukatili wa kijinsi kwenye kamati za Mtakuwwa kata hadi wilaya," alisema Mwesigwa.

Mwesigwa aliongeza: "Milioni 30 tulizopata kutoka The Foundation for Civil Society, milioni 25 zitatumika kwenye mradi huu, na milioni tano zitatumika kwenye utawala na elimu hii itatolewa kwa kushirikina na Ofisi ya Mganga Mkuu na Maofisa Afya.

Akipokea mradi huo, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya, Dk. David Lucas, alisema mradi huo umefika kwenye muda mwafaka na ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto na wanawake haupo kwa sasa, na endapo ukitokea atahakikisha wanaukomesha kwa kushirikiana na shirika hilo.

## Biteko aagiza kukamatwa wanaokiuka sheria za madini

**Na Lucas Raphael, TABORA**

SERIKALI imeagiza kukamatwa kwa watu wote wanaokusanya ushuru unaopingana na sheria za madini, kanuni na taratibu zilizowekwa na wizara hiyo ili iwe fundisho kwa wengine.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, alipokuwa akiongea na wachimbaji wadogo katika kijiji cha Isanga, wilayani Nzega, mkoani Tabora, jana.

Alisema kuwatoza ushuru wa Sh. 1,000 kila mfuko wa mawe ni kosa kisheria na yeyote anayefanya hivyo anastahili kukamatwa na kushtakiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema wenye leseni kuwatoza ushuru kupitia mfuko wa mawe kila siku ni uonevu mkubwa na katu serikali haiwezi kulifumbia macho jambo hilo.

"Watu wanaofanya hivyo eti kwa lengo la kuwatambua wapasua mawe ni uonevu usio vumilika kabisa na kama unataka kumtambua mtu basi wanaweza kumtambua kwa sura, kwa kuwa kila siku mtu huyo yupo hapo Isanga na anapasua mawe kwa ajili ya kujipatia kipato, jambo hilo liwe mwisho vinginevyo mkono wa sheria utafanya kazi yake," alisema Biteko.

Aliwataka wenye leseni za madini nchini kuhakikisha ushuru wowote watakaotoza udhibitiwe na ofisa madini mkazi au kutoka ofisi hiyo ili kupunguza malalamiko ya aina hiyo.

Alisisitiza kuwa serikali inapenda wananchi wake wanufaike kutokana na rasilimali za nchi yao na sio kunufaisha watu wachache.

Awali, wachimbaji hao walimlalamikia waziri huyo kwa kumwambia kwamba wamekuwa wakitozwa ushuru kwa kila mfuko wa mawe Sh. 1,000.

**"Watu wanaofanya hivyo eti kwa lengo la kuwatambua wapasua mawe ni uonevu usio vumilika kabisa na kama unataka kumtambua mtu basi wanaweza kumtambua kwa sura, kwa kuwa kila siku mtu huyo yupo hapo Isanga na anapasua mawe kwa ajili ya kujipatia kipato, jambo hilo liwe mwisho vinginevyo mkono wa sheria utafanya kazi yake," alisema Biteko.**

Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 26, 2020
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 14

**Ukatili 'unavyoliza' mabinti Mara likizo hii ya corona**



Ukurasa 13

Corona ilivyoisuka upya enzi ya utaalamu, dijitali duniani



Ukurasa 12

**Elimu ilivyo wachomoa wanawake talaka holela**

SAYANSI

NA DK FELICIAN B. KILAHAMA

# MISITU NI ZAIDI YA YOTE

•Ni kisima cha mvua, tiba tabianchi, mito, chakula, dawa

TANZANIA ina eneo lenye misitu takribani hekta milioni 48 ambayo ndani yake kuna mabilioni ya manufaa.

Kwa taarifa misitu ni chanzo kikuu cha mvua, ni makazi ya wanyama, ndege, wadudu, ndiko zinakotoka dawa, matunda na mboga.

Hata hivyo Watanzania wengi wanaelewa umuhimu wa rasilimali hiyo kwa kuzingatia zaidi misitu na miti. Lakini suala la ikolojia na umuhimu wake kwa maisha ya kila siku hawalielewi kikamilifu.



Vyura wa Kihans ni miongoni mwa viumbe wa ajabu duniani. Wanyama hawa wanazaa na hupatikana Tanzania pekee. **PICHA: MTANDAO**

### UMUHIMU KIIKOLOJIA

Mathalani, misitu inachangia sana usalama wa chakula hususani kuboresha udongo kwa kuongeza mbolea kupitia majani na mizizi. Pia kuzuia mmomonyoko wa udongo. Wakati huohuo, nyuki huongeza uzalishaji wa mazao na mavuno kuwa mengi, kupitia kurutubisha au kuchavusha maua (pollination).

Hili hufanyika kwa kutembelea maua ya mimea mbalimbali wakati wakitengeneza asali ambayo pia hutumiwa na binadamu kwa chakula, tiba na mambo mengi.

Misitu na nyuki ni rasilimali muhimu kwa sababu huleta manufaa kama mbao, nguzo, kuni, mkaa, dawa na chakula hasa matunda, mboga asilia, mafuta 'edible and essential oils'.

Aidha, misitu ina wadudu waliwao kama nzige, chavichavi. Ndiko kwenye asali, uyoga, mizizi ambayo ni chakula na dawa, nyama ya wanyama na ndege pori kwa uchache. Vilevile, rasilimali misitu na nyuki ni chanzo cha kipato kwa Watanzania wengi. Mathalani, mnyororo mzima wa mazao ya misitu unahusisha wafanyabiashara wakubwa, kati na wadogo.

### AJIRA MIJINI/VIJIJINI

Misitu ni ajira waliowengi mijini na vijijini wanajihusisha na usambazaji au uuzaji wa mazao ya misitu. Upatikanaji wa mkaa, kuni, nguzo, mbao, fito na asali kirahisi katika mitaa na sehemu tunazoishi ni matokeo ya wasambazi au wajasiriamali wa chini .

Kutokana na rasilimali misitu kuwa chanzo muhimu za bidhaa kadhaa na hatimaye kutupatia kipato ndiyo maana misitu hupewa jina la 'misitu ni mali."

Misitu imegawanyika katika sehemu kuu mbili za uhifadhi na uzalishaji mali kwa maana kwamba kupitia misitu-hifadhi tunapata huduma za kiikolojia na misitu uzalishaji tunapata bidhaa kwa matumizi mbalimbali.

Upatikanaji wa huduma za kiikolojia kwa njia endelevu ni jambo la msingi kwa maendeleo ya nchi na kila mmoja.

Mathalani, misitu na uoto wa asili kwa ujumla, husaidia kuhifadhi udongo ambao ni muhimu kwa uzalishaji wa chakula.

Vilevile, misitu na uotoasilia husaidia maji ya mvua kupenya ardhini kirahisi hivyo kuhifadhi maji ambayo hupatikana mwaka mzima kupitia chemichemi na mito.

### MBOJI ARDHINI

Kadhalika hurutubisha udongo kutokana na majani, matavi na baadhi ya miti kuanguka na kuoza hatimaye kuchanganyikana na udongo na kuwa mbolea.

Isitoshe kupitia baadhi ya miti ardhi hupata rutuba kwani mizizi yake hufyonza gesi ya naitrojeni na kuiingiza ardhini mchakato unaoitwa 'nitrogen fixation' na kuimarisha ukuaji wa mazao na mimea.

### MAKAZI YA BIYOANUAI

Kimsingi misitu huweka mazingira mazuri kwa biyoanuai au 'biodiversity` mbalimbali kuweza kuishi kwa mfano, wanyama na ndege mapori na nyuki pia kuwapo baadhi ya mimea na wanyama wasiopatikana sehemu nyingine duniani isipokuwa Tanzania pekee.

Kupitia mfumo huo taifa linanufaika kwa utalii pamoja na kuzalisha chakula cha kutosha aidha, hupata asali na nta ambayo ni huduma ya nyuki.

Kadhalika, mito yenye maji ya kutosha kama Rufiji, Ruvu, Ugala, Ruaha na Ruvuma ni zao la misitu.

Kupitia umwagiliaji watu wanapata chakula zaidi na ndicho chanzo cha umeme wa maji ambao ni muhimu kwa shughuli za viwanda, usafirishaji, biashara na uchumi.

Maji pia ni makazi na maisha ya wanyama kama viboko, mamba, samaki pamoja viumbe wengine kama vyura na wengineo waishio majini. Rasilimali zote hizo ni muhimu kwa manufaa ya raia na maendeleo ya taifa.

### KUBORESHA TABIANCHI

Kadhalika misitu na mimea husaidia kuboresha tabianchi kupitia uwezo wake wa kufyonza gesiukaa au 'carbon dioxide-CO2' kuitoa kwenye mfumo wa hewa na kuitumia kutengeneza chakula kinachowezesha ukuaji wake na wakati huo kuingiza oksijeni hewani kwa matumizi ya binadamu na viumbe hai wengine.

Pamoja na huduma zote hizo muhimu, binadamu tumekuwa mwimba kwa misitu kutokana na shughuli mbalimbali tunazozifanya bila kuzingatia matumizi endelevu kwa rasilimali misitu.

### MISITU KUTOWEKA

Takwimu za 2015 zilizotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii zilionyesha kuwa tunapoteza misitu ya asili kwa kasi ya hekta 372,000 kwa mwaka kutokana na shughuli za kibinadamu zisizozingatia uhifadhi na kilimo kijani. Vilevile, mwaka 2017 Kituo cha Taifa cha Kufuatilia mwenendo wa gesi kaboni na madhara ya tabianchi (National Carbon Monitoring Centre-NCMC) kilichopo Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), ilionekana kasi ya kutoweka misitu ilifikia hekta zaidi ya 469,000 kwa mwaka.

Hali hii inatokana na usimamizi usioridhisha kwa misitu ya asili hasa vijijini, hivyo kutokana na kilimo cha kuhamahama, kuvuna miti kiholela, kuchoma moto mapori, ufugaji usiozingatia wingi na uwezo wa eneo la malisho.

Pia kutokuwapo matumizi bora ya ardhi vijijini ni visababishi misitu kuharibika haraka. Kutokana na ripoti hizo inaaminika kuwa misitu ya Tanzania inaweza kutupatia meta za ujazo milioni 42.5 bila kuathiri ukuaji na kuendelea kutoa huduma za kiikolojia ipasavyo.

Lakini kiasi kinachovunwa kila mwaka ni takribani meta za ujazo milioni 62 kuashiria kuwa tunakata miti zaidi kwa meta za ujazo milioni

INAENDELEA UK.13

UCHAMBUZI
**NA BEATRICE PHILEMON**



Wanawake wa asasi isiyo ya kiraia ya haki za wanawake wilaya ya Tandahimba (Taworo), katika mkutano na maofisa wa ActionAid wakielezea mafanikio kiuchumi na kijamii. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

# Elimu ilivyowachomoa wanawake talaka holela

ELIMU ya uwajibikaji na utawala bora, kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na mabinti pamoja na haki za wanawake, imeanza kuleta mabadiliko kwa baadhi ya kina mama mkoani Mtwara.

Wanufaika wa elimu hiyo katika wilaya ya Tandahimba mkoani wanasema kuna mabadiliko kwa sababu umma unafahamu athari za unyanyasaji wa wanawake na watoto.

Kina mama wanasema kuna mabadiliko makubwa kwa wanawake na mabinti kwa sababu hivi sasa asilimia kubwa ya wananchi wanafahamu madhara ya ukatili wa kijinsia , unyanyasaji watoto na cha kujivunia mimba za utotoni zimepungua.

"Wanawake wameanza kutoa uamuzi wa maendeleo mbalimbali katika ngazi ya familia, ikiwamo kutoa maoni kwenye mikutano ya wanavijiji kitu ambacho awali kilikuwa hakiwezekani," anasema Ofisa Maendeleo ya Jamii na Mratibu Dawati la Jinsia la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba, Neema Shungu.

Akizungumzia mafanikio hayo anasema ni ushirikiano na wadau mbalimbali wakiwamo Shirika la Actionaid Tanzania katika wilaya ya Tandahimba. Anaeleza kuwa elimu hii iliyotolewa kupitia mradi wa ' Local Rights Programmes' (LRP), imekuwa na mafanikio makubwa katika jamii zilizofikiwa.

"ActionAid Tanzania ni wadau wetu wakubwa wa kumkomboa mwanamke na binti ili kupata haki zao, tunawaomba wasonge mbele kusaidia akina mama na watoto katika maeneo mengine ya Mtwara," anasema Shungu.

> "Watoto wa kike wanajitambua. Mimba zimepungua sana na idadi ya wanafunzi wanaopata mimba imeshuka kutoka 54 mwaka 2018 hadi kufikia wanafunzi 15 mwaka huu ambayo ni sawa na asilimia 0.04.

"Wanawake wanajua maana ya ukatili wa kijinsia, madhara ya ukatili huo kwa watoto na familia kwa ujumla," anaongeza.

### MIMBA KUPUNGUA

Shungu anaeleza kuwa mbali na hilo, idadi ya watoto wa kike wanaoshindwa kusoma kutokana na mimba za utotoni imepungua na hivi sasa wazazi wengi wanaelewa umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike tofauti na miaka ya nyuma.

"Watoto wa kike wanajitambua. Mimba zimepungua sana na idadi ya wanafunzi wanaopata mimba imeshuka kutoka 54 mwaka 2018 hadi kufikia wanafunzi 15 mwaka huu ambayo ni sawa na asilimia 0.04," anasema Shungu.

Anaeleza kuwa kupitia mradi wa 'Local Rights Programme' wanawake katika wilaya ya Tandahimba walifundishwa kwa undani masuala ya ukatili wa kijinsia, madhara yake, haki za wanawake katika masuala ya elimu, kumiliki ardhi, ndoa, mirathi, elimu ya ujasiliamali, athari za mimba za utotoni na haki za watoto.

Aidha, walifundishwa jinsi ya kufuatilia miradi ya jamii inayotekelezwa katika maeneo yao na kuangalia thamani halisi ya fedha ikilinganishwa na miradi.

### MAFANIKIO ZAIDI

Mratibu Shungu anasema elimu hiyo ilitolewa na ActionAid Tanzania kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kupitia Idara ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii.

" Elimu hii imeleta mabadiliko makubwa katika wilaya yetu kwa sababu hivi sasa tumeanza kuona wanawake wamejitambua. Wanaweza kujitetea na kudai haki zao mahakamani. Watoto wao wanaishi vizuri, talaka zimepungua, wanaweza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi wa siasa katika ngazi ya vijiji na kata kitu ambacho kilikuwa hakiwezekani katika miaka ya nyumba." Anakumbusha.

Anasifu kuwa mbali na hilo, hivi sasa wanawake wana ujasiri wa kujadili masuala mbalimbali yanayochochea ukatili wa kijinsia ikiwamo elimu kwa mtoto wa kike na haki zake katika ngazi ya shule na baadae kuwasilisha changamoto hizo kwa ofisa wa dawati la jinsia .

### UJASIRIAMALI

Akizungumzia elimu ya ujasiliamali, anasema kwa upande wa elimu ya ujasiriamali wamekuwa wakienda kwenye mikutano ya vijiji ili kutoa mafunzo kwa kina mama wa mtaani na kuwaambia fursa za biashara zilizopo, lengo ni kuwasaidia kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine," alisema.

Pia wanaotakiwa kupata mikopo wanapewa elimu ya ujasiliamali kwanza kabla ya kuchukua mkopo ili watumie fedha hizo vizuri na wasitumie kwa kuoa.

"Kwa vikundi vinavyokopeshwa na halmashauri, tuna darasa maalumu kwa ajili yao," anaongeza Shungu.

Anaeleza kuwa kwa upande wa vijana anasema vijana 60 wenye umri kati ya miaka 20-24 kutoka maeneo mbalimbali ya Tandahimba walipata mafunzo ya ufugaji wa kuku kwa kushirikiana na Taasisi ya Aga Khan Foundation, na baada ya mafunzo walipewa mtaji wa kukuna kunufaisha vijana kutoka kata 32 za wilaya hiyo.

Mbali na hilo, shirika la Voluntary Service Overseas (VSO) kupitia mradi wake wa kuwasaidia na kuendeleza wajasiliamali Tanzania (TLED) limetoa mafunzo kwa vikundi 100 vya kina mama.

Shungu anasema kina mama wengi wanaweza kuwa na mitaji ya biashara lakini changamoto kubwa ni jinsi ya kutumia mitaji hiyo.

"Tunawashukuru wadau Actionaid, TLED na wengine kwa msaada wa kuelimisha jamii ili kumkomboa mwanamke na kupunguza umaskini. Aidha, ni nguzo ya kumkomboa mtoto wa kike katika masuala ya elimu, kupinga ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake na kuwezesha watoto kufurahia haki zao ikiwamo kupata elimu," anasema.

Kupitia elimu hizi na mikutano hii angalau kesi za kuvunjika kwa ndoa zimepungua, ukienda kitengo cha jamii kwenye dawati la jinsia, kesi zimepungua sana kwa sababu jamii imeelewa na kuona kuwa safisha ghala ni ujinga mtupu.

Anasema mbali na hilo, ukiukwaji haki za wanawake na mtoto ikiwamo ukatili imepungua kwa kiasi na sisi kama halmashauri tunajitahidi kwenda kwenye mikutano ya vijiji kutoa elimu kwa ajili ya kupinga ukatili wa kijinsia na mimba za utotoni.

Anasema kabla ya mafunzo, maisha ya wanawake na watoto wa kike yalikuwa mabaya, wanawake wengi hawakujua haki zao, Walitelekezwa na waume zao hasa bila kuwa na kitu chochote hasa katika kipindi cha msimu wa mavuno ya korosho na pia watoto wa kike walilazimishwa kukaa nyumbani kwa ajili ya shughuli za nyumbani au kuolewa bila ridhaa yao.

Mratibu wa Actionaid Wilaya ya Tandahimba na Newala, Dinno Kamonalo, anasema kina mama namabinti wana ujasiri wa kufanya shughuli za aina mbalimbali na kushiriki kwenye mipango ya maendeleo. Mbali na hilo wanadai haki zao popote hata mahakamani na wanashiriki kwenye masuala ya familia hasa mambo yanayohusu mapato na matumizi.

Katibu wa Umoja wa Wanawake wa Tandahimba (Taworo) Rehema Hamis anasema , " tunashukuru uhamasishaji umetufumbua macho mambo mengi tulikuwa hatuyajui na tunateseka sana."Sasa tumejikwamua kiuchumi na kulisha familia zetu, zamani mwanamke alikuwa na hela lakini hatoi, pia wanawake wengi walikuwa wanaachika, hawajui haki zao," tuko vizuri

Akitoa ushuhuda jinsi alivyonufaika na mafunzo hayo, Ashura Manjapa kutoka kijiji cha Mnyawa wilayani humo anasema Actionaid amewapa elimu ya kudai haki, ujasiliamali, ubunifu kibiashara na yote yamechangia kwa kiasi kikubwa wanawake katika wilaya ya Tandahimba kujikwamu." Anasema.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Corona ilivyoisuka upya enzi ya utaalamu, dijitali duniani

UKIFUATILIA jinsi vijana shuleni na vyuoni wanavyochagua maeneo wanayotaka kusomea, utakuta kuna kitu kama mikondo ya kitaaluma inayotokana na mazingira ya kiuchumi na hata kisaikolojia ya wakati huo.

Itakumbukwa kuwa wakati wa miaka ya mwisho ya ukoloni fani zilizokuwa zinashindana zilikuwa chache. Kukawa na mijadala ya kifalsafa kwa kiwango fulani, kipi bora kijamii kati ya udaktari na ualimu, au uuguzi.

Kulikuwa na fani nyinginezo lakini hazikuwa katika mjadala, kwani zilikuwa na picha ya kuwa za hali ya chini, na siyo za kukimbilia, kwa mfano sekta pana ya ulinzi na usalama, yaani jeshi na ulinzi na polisi. Maeneo hayo yalianza kuonekana kuwa fani za kawaida miaka ya baadaye wakati mazingira ya kimaslahi yanabadilika na uthabiti wa ajira pamoja na matazamio mengine unaanza kupewa kipaumbele.

Fani za kibiashara kimsingi zilikuwa hazipo na hata katika shule masomo ya biashara yameingia katika mitaala baadaye, uchumi ulipobadilika. Fani ya biashara ilikuwa inafundishwa pembeni katika vyuo baada ya masuala ya mwanafunzi kuhitimu kiwango fulani cha elimu, au apate ushauri huo kutokana na 'careers master,' mwalimu mshauri wa fani za ajira katika shule za sekondari.

Mapema zaidi, wanafunzi wanaohitimu darasa la nane walikuwa wanapata ushauri wa aina za ajira wanazoweza kufuatilia au kuomba kujiunga nazo, kulingana na walivyokuwa wanapenda michepuo fulani. Miaka ya karibuni watoa elimu wameacha kutoa ushauri kama huo kwani 'mpango mzima' sasa ni kuajiri, kujikita mahali.

Licha ya kuwa michepuo ya ajira imesinyaa ukilinganisha na wakati uliopita, bado vijana inabidi wafanye uamuzi wanataka kusoma nini vyuoni, na hata katika kujiunga na vidato vya juu mwelekeo wa masomo unaamua hatma au mvuto wa ajira baadaye. Tofauti na nyakati za awali ambako vijana walikuwa wanasoma huku wana uhakika wa kujiunga na fani hizo, mazingira ya sasa ni ya kubahatisha, kuwa anasoma ili ukipatikana mwanya apenye. Kama hajasoma hana uelekeo wa kuajiriwa ila kusaidia maeneo yanayohitaji nguvu kazi, hasa kwa sulubu na misuli.



Mfanyakazi akifanyia kazi nyumbani badala ya kujazana ofisini kuepusha maambukizo ya corona. **PICHA: MTANDAO**

> Licha ya michepuo hiyo katika ngazi za ajira ndogo ndogo za mtaani, janga la corona kwa jumla linaathiri kila sekta, iwe ni elimu au biashara, viwanda, utalii na kadhalika.

Kipindi hiki cha janga la corona kimeleta mazingira tofauti katika ajira, kwani kuzuia watu wasikae kwa makundi kulilazimisha wengi kuanza kufanyia kazi nyumbani, ila ni pale ambapo wanasimamia ajira hizo wao wenyewe, au waajiri wao wanawahitaji kuendelea kutumika.

Nyingi kati ya kazi hizo ni za kitaaluma, wakati baadhi ya kazi za sulubu zimetoweka au zinafanywa kwa njia nyingine, kutumia mawakala wanapokea orodha ya mahitaji ya wateja tofauti kutoka pembe tofauti za nchi, wanayafanyia kazi.

Jitihada ya kutokuwa pamoja katika makundi imesukuma mbele matumizi ya mitandao kama njia ya kuwasiliana hata kiofisi, siyo kijamii kama awali. Biashara inakuwa na kidijitali zaidi kuliko mwanzo, na baadhi ya taasisi zinachukua hatua kulinda amana zao wakati huu wa kuhamia dijitali, mara nyingine wakiwa wadau wa awali wa sekta ya kufanya biashara kidijitali lakini sasa inawaletea homa. Badala ya kuwa 'mkono wa ziada' kwa mfano ATM zilivyowasaidia watoa fedha dirishani katika mabenki mawakala wanachukua nafasi ya ATM ni rafiki zaidi kwa mteja.

Kwa maana hiyo kuna msukumo sasa kwa vijana kusoma masuala ya teknolojia mawasiliano au teknohama (teknolojia ya habari na mawasiliano) kama njia ya kuingia katika sekta tofauti za biashara au ajira.

Teknolojia hiyo inakuwa kiungo cha fani na anayeitaka fani hiyo, kwani kila mahali watu wanahitaji kutumia simu za mkononi kuwasiliana na wengine, kwa masuala yoyote yale kwani mizunguko imezuiliwa au haihitajiki katika wakati huu.

Uwakala katika biashara unakuwa rahisi zaidi mtu akiwa anamudu kutumia simu 'janja' za mkononi kwa mahitaji tofauti.

Imefikia mahali hata elimu sasa inaanza kufikiriwa kuwa itatolewa kwa njia endeleo endapo itahamia katika teknohama, yaani kwa njia ya mtandao na hivyo kufundisha wanafunzi walio nyumbani au katika vikundi vidogo.

Bado hakuna mfumo wa kuratibu hali hiyo na kwa jumla sekta ya elimu imekuwa ikingoja hali ya maambukizo ya corona nchini kutulia ili wanafunzi warudi shuleni na masomo yaendelee kama kawaida. Tatizo ni kuwa corona inaweza kuja kwa mawimbi, hivyo katika wakati ujao shule zifungwe tena, na njia mbadala zianze kufuatiliwa.

Endapo itafikia wakati mazingira ya kijamii yabadilishwe wanafunzi wapate nafasi za kusoma katika 'fremu' kama za maduka au vyumba mitaani mahali panapoaminiwa, na hata vibwalo vya hapa na pale endapo wanaweza kukaa kwa nafasi, utaalamu wa teknohama utashamiri.

Licha ya kuwapo mwalimu mwelekezi na hata mara nyingine mwanafunzi tu ambaye labda alishamaliza kidato hicho na yuko hapo mtaani, ashirikiane na fundi (mtaalamu kiasi) wa teknohama kuweza kufikisha mtiririko mwa masomo ya kidato fulani au chuo, kwa kutumia 'app' zitakazozagaa tu.

Licha ya michepuo hiyo katika ngazi za ajira ndogo ndogo za mtaani, janga la corona kwa jumla linaathiri kila sekta, iwe ni elimu au biashara, viwanda, utalii na kadhalika.

Hata pale nchi zinapojitahidi kufungua tena shughuli hizo, bado mazingira ya tahadhari yanazuia kukua kwa shughuli hizo, na hasa kukwamisha uwekezaji kutokana na giza nene kuhusu kupatikana faida katika wakati unaoweza kupimika. Huwezi tena kuona mahoteli yakijengwa ila kwa taabu, au kununua mlolongo wa magari ya utalii, n.k. Ni kuboresha mawasiliano kuendesha kile kilichopo.

# Misitu ni zaidi ya yote

**INATOKA UK.11**

19.5 kuliko kiwango kinachotakiwa kuvunwa bila kuathiri misitu.

**UFUMBUZI**

Inabidi kujizatiti kuisimamia misitu kwa nia ya kuhakikisha nchi inavuna kiwango kinachotakiwa kuvunwa na siyo kinyume chake.

Kinachotakiwa ni kuhakikisha huduma za kiikolojia zinadumishwa kwa faida ya wote. Mkazo uwe kwa upatikanaji, utumiaji sahihi na uendelezaji wa huduma husika mahali. Kilimo kiwe kijani na endelevu pia ufugaji uzingatie uwezo wa malisho na panapowezekana wafugaji wamilikishwe maeneo ya kuchungia na wayaendeleze kwa kufuata ushauri wa wataalamu.

Ili kufanikisha yote ni vizuri kukawepo ushirikiano wa karibu kwa sekta na taasisi husika kuanzia serikali kuu, za mitaa hadi utawala wa vijijini bila kusahau wadau wengine muhimu na jamii.

Kwa sasa dunia imeghubikwa na taharuki ya mlipuko wa COVID-19, kila mahali duniani ni kilio cha athari zake kwa maisha na uchumi wa nchi husika, siyo hilo tu bali pia kulaumiana na kunyosheana vidole na kuchukiana kwa kukosa huduma watu walizozizoea.

Kwa upande mwingine tumekumbushwa kuwa misitu ndiyo hazina na chanzo cha dawa nyingi zinazotibu maradhi mbalimbali. Wazazi wetu na mababu walitumia sana mitishamba walikuwa hawana huduma za kiafya kama ilivyo sana lakini waliishi miaka mingi.

Kiuhalisia misitu ni kiwanda cha dawa tuitunze na iweze pia kututunza.

**Mwandishi ni Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki mstaafu.**

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

# Ukatili ‘unavyoliza’ mabinti Mara likizo hii ya corona



IGP Sirro (katikati), akiwa na wanafunzi na wadau wengine kuzindua dawati la jinsia na watoto wilayani Butiama mwaka jana. **PICHA: JESHI LA POLISI**

KWA jinsi hali ilivyo kwenye baadhi ya maeneo nchini, huenda hadi shule kufunguliwa, wanafunzi wengi watakuwa wameshaumia kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo kukeketwa, mimba na ndoa za utotoni.

Hii ni kutokana na waathirika 47 wakiwamo wanafunzi 29 wa msingi na sekondari, wilayani Serengeti wanaokimbia makwao kukwepa ukatili huo. Mbali na hao wapo watoto 18 wamekimbia visu vya ngaruiba mkoani Mara.

Wote kwa sasa wanatunzwa katika kituo cha nyumba salama kilichopo mjini Mugumu.

Wanafunzi hao waliokolewa katika operesheni maalumu inayoendelea wilayani humo iliyoanza Aprili mosi mwaka huu, kwa lengo la kuwaepusha wanafunzi hao na vitendo hivyo hatari.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo, Rhobi Samwelly, uokoaji huo wa wanafunzi unafanywa na shirika lake kwa ushirikiano na vyombo vya dola na wadau wengine wa kupinga ukatili wa kijinsia.

**MKAKATI**

Mkurugenzi Rhobi anasema, wanafunzi wanatolewa maeneo mbalimbali ya vijiji vya Serengeti na kufikishwa katika kituo hicho, wamekuwa wakihamishwa shule au kurudi kwa wazazi wao lakini kwa makubaliano maalumu.

“Tunataka mtoto wa kike asome, hivyo huwa tunashirikiana na watu wa idara ya elimu kupata uhamisho wa muda ili tujenge uhusiano mzuri na wazazi wa wanafunzi kwanza,” anasema.

> “Serengeti ina shule za msingi 128, sita kati ya hizo zikiwa za binafsi, lakini matukio mengi ya ukatili yanatokea katika shule za vijijini, na wanapoletwa mjini Hope wanakuja kuwaombea uhamisho.

Anafafanua kuwa wale ambao wazazi wao wanakubali kuwapokea na kuahidi kutowakeketa, huwa wanaruhusiwa kurudi kwao, lakini wanaokataa kuwapokea, inabidi wahamishiwe shule za mjini Mugumu.

“Huo ndiyo utaratibu tunaoutumia siku zote tangu kituo cha nyumba salama kilipoanzishwa, na wapo wanafunzi wanaokataa kurudi kwao wakihofia kukeketwa, hatuwezi kuwalazimisha,” anasema.

Anaongeza kuwa kwa wanafunzi waliohitimu au kutobahatika kusoma, kuna mafunzo ya ujuzi ukiwamo ushonaji wa nguo, kufuma vitu mbalimbali ili baadaye ujuzi huo wautumie kuendesha maisha yao baadaye.

Rhobi anasema, mtoto wa kike si wa kukeketwa au kuolewa au kukeketwa ili kufaidisha watu, bali anatakiwa kusoma kama ilivyo kwa mtoto wa kiume, ndiyo maana shirika lake liko mstari wa mbele kuhakikisha anapata elimu.

Anasema, kituo cha nyumba salama cha Mugumu, kwa sasa kina wasichana 110 wakiwamo hao wapya 47 waliookolewa hivi karibuni, huku juhudi za kuokoa wengine zikiendelea.

**SABABU ZA UNYANYASAJI**

Juhudi mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa jamii, vimekuwa vikifanyika ili kukomesha vitendo vya ukeketaji na hata ndoa za utotoni nchini, lakini bado vinaendelea kuwapo kwenye baadhi ya maeneo.

Inaelezwa kuwa sababu kubwa ya kuendelea kuwapo kwa vitendo hivyo ni kutokana na faida inayopatikana, kwa vile msichana anakeketwa kwa Sh. 30,000.

Katika kiasi hicho cha fedha, 20,000 ni ya ngariba na 10,000 ni ya wazee wa kimila, wakati mzazi anayemtoa binti yake akeketwe, faida yake ni ng’ombe anazopata baada ya kuozesha binti .

Kwa mujibu wa ngariba mstaafu Muhabe Marwa, anayeongeza kuwa yote ni mateso kwa mtoto kwa binti ambaye kama angeachwa asome elimu ingemuokoa.

“Niliacha ungariba baada ya kuelimishwa na wadau wanaopinga ukeketaji wa Hope for Girls and Women Tanzania, hivyo tusichoke kuelimisha jamii inayokumbatia mila hizi potofu, zinazokwamisha maendeleo ya mtoto wetu,” anasema Muhabe.

Muhabe anasema, ukeketaji unaendelea kwa sasa wakati huu ambao shule zimefungwa, kwa vile wahusika wanajua mwezi wa ukeketaji ambao ni Desemba, hata vyombo vya dola vinaujua.

“Kuendelea kwa vitendo vya ukeketaji wilayani kwetu ni kutokana na kuendekeza mila potofu na tamaa ya kutaka kujipatia fedha kwa njia zisizo halali, ndiyo maana mimi nilielimishwa nikaacha,” anasema.

**WADAU WA ELIMU**

Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya ya Serengeti, Simon Mdaki, anasema, wale wote wanaozingatia Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978 hawawezi kukwamisha maendeleo ya elimu ya mtoto wa kike au wa kiume.

Anasema, miongoni mwa vipaungele vya sheria hiyo ni kwamba ni marufuku kwa mwanafunzi kuoa au kuolewa, hivyo kwa namna yoyote ile mwanafunzi hatakiwi kukwamishwa katika elimu.

“Ukeketaji na ndoa za utotoni vinamkwamisha elimu, nasi suala hili tumalikomea kwa nguvu zote na ndiyo maana tukawa na kamati ya ulinzi wa mtoto kila kijiji,” anasema Mdaki. “Kamati hizo zinasaidia kutoa taarifa za vitendo vya ukatili, pia walimu wa shule zote 40 wanaelimisha wanafunzi kuhusu vitendo hivyo, ili wanapotaka kufanyiwa vitendo hivyo wanatoa taarifa kwenye kamati,” anasema

Ofisa Elimu ya Msingi wa wilaya hiyo, Ally Almas, anasema, idara yake ina ushirikiano mzuri na shirika la Hope for Girls and Women Tanzania kwa lengo la kusaidia wasichana kusoma.

“Serengeti ina shule za msingi 128, sita kati ya hizo zikiwa za binafsi, lakini matukio mengi ya ukatili yanatokea katika shule za vijijini, na wanapoletwa mjini Hope wanakuja kuwaombea uhamisho,” anasema Almas.

Anasema, lengo ni kuhakikisha wanaendelea kusoma, hivyo idara yake inashiriki kikamilifu kuhakikisha wanafunzi hao wanapata uhamisho wa muda wakati juhudi nyingine zikiendelea au kuhamishwa moja kwa moja.

Wilaya nne za Serengeti, Bunda, Butiama na Tarime zina madawati ya jinsia yaliyozinduliwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini IGP Simon Sirro, mwishoni mwa mwaka jana.

Sirro aliwataka wananchi kuacha kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili, jambo linalosabisha ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Alisema polisi haiwezi kuvumilia mambo yaliyopitwa na wakati lazima wanaoyafanya wakiwamo wanaume wanaoendeleza ubabe kwa wake zao kuadhibiwa kisheria.

“Kina mama lindeni watoto wenu, wazazi wangu wasingenilinda nisingekuwa IGP . Hujui mtoto wako atakuwa nani baadaye na nyie wababa msiwarubuni watoto wadogo,” anaonya IGP Sirro.

Aidha, anawataka wasichana wasikubali kurubuniwa na vitu vidogo vinavyoharibu ndoto zao na wakiona kuna viahashiria vya mtu mzima kuwahadaa au kuwataka kimapenzi watoe taarifa kwenye dawati la jinsia.

Lengo la kuwapo kwa madawati hayo, ni moja ya harakati za kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto ikiwamo ukeketaji, mimba, ndoa za utotoni na ukatili mwingine ndani ya jamii au familia.



# Wanaoamini pombe inaua virusi corona waonywa

**Renatha Msungu, DODOMA**

UELEWA mdogo na imani potofu ya mlipuko wa ugonjwa hatari wa homa ya mapafu unaotokana na maambukizo ya virusi vya corona (Covid-19), maeneo ya vijijini umeleta ongezeko la unywaji wa pombe kwa imani kuwa inazuia maambukizo hayo.

Akizungumza juzi wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji na wanajamii yaliyotolewa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la Action Aid, katika Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, Mtendaji wa Kijiji cha Nzali Benedict Noti, alisema katika maeneo ya vijijini watu wengi wanatumia pombe za kienyeji kwa kisingizio kuwa inaua virusi vya corona.

"Unywaji pombe umeongezeka sana vijijini kwa hofu ya kujikinga na corona," alisema.

Alisema kutokana na mazingira hayo wana kazi kubwa ya kuwafikia wananchi ili kubadili mtazamo na kuwa waangalifu zaidi katika vita dhidi ya corona.

"Serikali inajitahidi kwa upande wake kwenye suala la kutoa elimu kinachotakiwa ni kuendelea kuelimisha wananchi kuwa matumizi ya pombe sio njia sahihi za kujikinga na corona na wanachotakiwa kufanya ni kuchukua tahadhari," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Jukwaa la Wakulima Wadogo Wanawake Chamwino (JUWWACHA), Janeth Nyamayahasi, alisema, lazima elimu iendelee kutolewa vijijini ili watu wauelewe ugonjwa na kuangalia tahadhari zinazotolewa na wataalamu wa afya.

"Elimu iendelee kutolewa vijijini kwenye jamii zetu, wengi wanaamini ugonjwa huu uko mijini, kuna mikusanyiko bado inaendelea, watu hawana hofu ya ugonjwa mfano walevi wamekuwa wakichangia kikombe kimoja cha pombe," alisema.

Utoaji elimu uliozinduliwa na Action Aid unafanyika kwa pamoja kwa ushirikiano na serikali.

Wanachofanya Action Aid ni kuwajengea uwezo viongozi wa serikali.

Katika mafunzo hayo mwezeshaji, Dk. Stephen Mwaisombwa, alieleza umuhimu wa kufuata tahadhari zilizotolewa na Wizara ya Afya na pia haja ya matumizi ya nguo za kulinda mtoa huduma (PPE).

**"Elimu iendelee kutolewa vijijini kwenye jamii zetu, wengi wanaamini ugonjwa huu uko mijini, kuna mikusanyiko bado inaendelea, watu hawana hofu ya ugonjwa mfano walevi wamekuwa wakichangia kikombe kimoja cha pombe," alisema.**

# Umaki yasaidia vifaa vya corona mil. 6/-

**Na Paul Mabeja, MANYONI**

USHIRIKA wa Mama wa Kikristo (Umaki) wa Kanisa la Anglikana Tanzania, umetoa msaada wa vifaa vya kujikinga na virusi vya corona vyenye thamani ya Sh. milioni sita, kwa familia maskini katika Kijiji cha Sukamahela, wilayani Manyoni mkoani Singida.

Mratibu wa Umaki, Magreth Massawa, alisema msaada huo ni sehemu ya kuunga juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya virusi vya corona nchini.

Alisema kutokana na vifaa vya kujikinda na maambukizo ya corona kuwa na gharama kubwa, wameona Umaki kuchangishana na kupata fedha kwa ajili ya kusaidia familia hizo maskini.

"Barakoa moja yenye kiwango inauzwa hadi Sh. 3,000, hivyo kwa hizi familia duni zisingeweza kumudu gharama hizi, hivyo kushindwa kujilinda na maambukizo ya virusi vya corona," alisema Massawa. Pia, wametoa kwa kila mtu kilo tano za unga wa sembe kwa ajili ya chakula.

"Watu ambao tumewapatia msaada ni zaidi ya 100 kijijini hapa tumetoa ndoo za kunawia mikono, sabuni, vitakasa mikono, barakoa, lakini tumeona tusiishie kutoa vifaa tuu pamoja na elimu, lakini tumewapatia chakula ambao ni unga wa ugali ili waendele kujikimu katika kipindi hichi," alisema.

Naye Mbunge wa Manyoni Mashariki, Daniel Mtuka, alisema kuwa vifaa hivyo vimekuja wakati mwafaka kwa kuwa mahitaji bado ni mengi katika eneo hilo.

"Nitoe rai, pia kwa watu pamoja na mashirika mengine watusaidie vifaa hivi ili wananchi wetu wanapokuwa wanaendelea na majukumu, pia wawe wamejilinda," alisema Mtuka.

Vile vile, aliwataka wananchi kuacha kubweteka katika kipindi hiki serikali imetangaza kufungua baadhi ya shughuli kwa kuwa virusi vya corona bado vipo na vinaendelea kuua.

"Nawaomba Watanzania wenzangu tusibweteke kwa kufikiri kuwa gonjwa hili limepita bali tuendelee kuchukua tahadhari zote zinatolewa na wataalamu wa afya," alisema.

Mwakilishi wa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Dk. Frednand Kutimwa, alisema wanaendelea kutoa elimu kwa jamii katika maeneo mbalimbali ili kujikinga na virusi vya corona.



Mkazi wa Kijiji cha Bahi, mkoani Dodoma, akijenga choo jana, kwa kufunika kwa miti ili kukabiliana na magonjwa ya mlipuko yanayosababishwa na ukosefu wa huduma hiyo muhimu. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Watoto kaya maskini kupata kadi NHIF bure

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WATOTO 148 katika baadhi ya kaya maskini nchini, wanatarajia kupatiwa kadi za bima za afya (NHIF) bure kwa ajili ya matibabu na Shirika lisilokuwa la kiserikali SACHIA Society ikiwa ni kuunga mkono juhudi za serikali za kutoa huduma za afya kwa wananchi wake.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Utawala wa Shirika hilo, Nsia Paul, wakati alipozungumza wakati wa kutoa kadi hizo kwa awamu ya pili kwa watoto 70 wa Kata ya Makutupora, jijini hapa juzi.

Paul, alisema mpaka sasa watoto 148, wamepatiwa kadi hizo za bima ya afya kutoka kaya maskini hapa nchini ikiwa ni juhudi za taasisi hiyo kuunga mkono juhudi za serikali kutoa huduma hiyo kwa watu wake.

Alisema katika idadi hiyo ya watoto 148, watoto 103 wanatoka mkoani Dodoma, huku wengine 45 wakitoka Dar es Salaam.

Pia alisema taasisi hiyo inafanyakazi katika Mkoa wa Pwani kwa kusaidia watoto 28 wanaoishi kwenye mazingira magumu na hatarishi na lengo lao ni kuwafikia wengine zaidi katika mikoa mingine kutokana na bajeti itakavyoruhusu.

Alisema kutokana na serikali kuhamishia makao makuu yake jijini Dodoma na Shirika hilo tayari limefungua rasmi makao yake makuu jijini hapo ili kuunga mkono serikali.

Kadhalika alisema taasisi hiyo ilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma bure kwa makundi ya watoto wenye umri kati ya miaka saba hadi 17 ambao ni yatima, wenye ulemavu wa viungo na ngozi.

Wengine wanaolengwa na taasisi hiyo ni wenye mtindio wa ubongo, waliotelekezwa, wanaoishi katika kaya maskini na wasichana waliokosa nafasi ya kujiendeleza kielimu kwa kushindwa kuhitimu elimu ya msingi na sekondari.

Paul alisema shirika hilo limekuwa likitoa elimu ya kuwajengea uwezo wa uchumi kinamama wa familia za watoto waliopewa kadi kwa lengo kuondokana na utegemezi wa wafadhili.

Kuhusu kundi la wasichana waliokatisha masomo, alisema wamekuwa wakijengewa uwezo wa elimu ya ujasiriamali ili kujitambua katika kuzalisha mali.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Taasisi hiyo, Kanda ya Kati Dodoma, Elizabeth Kimwage, alisema mkoani hapa wanafanyakazi katika Kata ya Makutupora kwa sababu ni eneo la nje ya mji na ndipo wanapopatikana walengwa wengi.

Kimwage aliitaja mitaa kwenye kata hiyo ambayo watoto wake 103 waliokabidhiwa kadi na taasisi hiyo kuwa ni Azimio, Vyeyula, Makutupora, Mchemwa, Mmbande, Namihanga, Kambarage, Mji Mpya na Sekondari.



HABARI MBEYA

# Wakulima wadogo wapewa siri kukua

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAKULIMA wadogo wameshauriwa kuzingatia matumizi ya teknolojia bora za kilimo na kuachana na kilimo cha mazoea ili wakue na kuwa wakulima wakubwa badala ya kuendelea kujiita wadogo.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa akizungumza na teknolojia za kilimo ambazo taasisi hiyo imebuni.

Alisema wakulima wanatakiwa wazalishe kwa kufuata utaratibu wanaoelekezwa na wataalamu wakiwamo maofisa kilimo wa vijiji pamoja na wataalamu wanaouza pembejeo za kilimo.

Alisema taasisi hiyo haitaki watu kuendelea kujiita wakulima wadogo wakati teknolojia zipo nyingi, na kwa sasa hivi wamekuja na teknolojia ya kupima udongo na kuwashauri wakulima mazao yanayofaa kulingana na aina ya virutubisho.

"Kwa sasa serikali inapambana kuingia kwenye uchumi wa viwanda ambao unahitaji malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda vinavyoanzishwa, sasa tukiendelea kuwa na wakulima wadogo wengi haitatusaidia," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisisitiza kuwa maofisa kilimo wa vijiji wanatakiwa kuanzisha utaratibu wa kufuatilia ukuwaji wa wakulima kwenye maeneo yao ili kuepuka kuwa na wakulima ambao hawakui kila mwaka.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wakulima katika maeneo mbalimbali kuzalisha mazao ya kimkakati kwa kutumia mbegu za kisasa zinazozalishwa na taasisi hiyo, ili wainuke badala ya kuendelea kuwa vile vile huku baadhi wakitumia mbegu za kienyeji.

Dk. Bucheyeki alisema taasisi hiyo imezalisha mbegu mbalimbali za kisasa ambazo wakulima wanashauriwa kuzitumia ili kuongeza tija zikiwemo za maharage, mahindi, alizeti, maparachichi na ngano.

Mtafiti wa zao la viazi mviringo katika taasisi hiyo, Dk. Dolla Mende, alisema katika utafiti wamegundua mbegu ambazo zikitumiwa na wakulima zitawainua kutokana na kuzaa vizuri na kukinzana na magonjwa pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema wameshazalisha aina 10 za mbegu za viazi na kwamba aina zingine zipo kwenye hatua mbalimbali za utafiti ili kuangalia ubora wake na kama zitafaa zitasambazwa kwa wakulima ili waendelee kuzizalisha.

# Matukio 16 ukatili kijinsia yaripotiwa kwa miezi mitatu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JUMLA ya matukio 16 ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mkoani Mbeya, yameripotiwa katika kipindi hiki cha janga la maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu.

Taarifa hiyo, iliyotolewa na Mratibu wa Chama cha Wasaidizi wa kisheria Mbeya (Mbepace), Laiki Ndagile, wakati akizungumza na Nipashe juu ya mwenendo wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kipindi hiki cha janga la corona.

Alisema kwa mujibu wa utafiti, walibaini ongezeko la vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu katika kipindi hiki ambavyo haviripotiwi popote kwa hofu kwamba wakitoka wanaweza pata maambukizo ya corona.

Alidai hofu hiyo imesababisha makundi mbalimbali ya watu wachukue tahadhari ya kutotembea ikiwa ni pamoja na kwenda kutolea taarifa za uvunjifu wa haki katika vyombo vinavyohusika ikiwamo Mahakama na Polisi.

Alisema waathirika wa vitendo hivyo ni wanawake ambapo kwa takwimu ni kwamba jumla ya wanawake 15 na mwanaume mmoja walifanyiwa ukatili.

Alifafanua kuwa Wilaya ya Kyela idadi ya waliofanyiwa ukatili katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi ni wanne, Chunya wawili, Mbarali wawili, Rungwe mmoja na Wilaya ya Mbeya saba.

"Wanawake na watoto ndio waathiriwa wakubwa wa ukatili huu wa kijinsia hasa kutoka jamii za kifugaji ambazo zinapatikana wilaya za Mbeya, Mbarali na Chunya, mbali na hayo ipo hofu kubwa zaidi kwa mabinti kutokana na kufungwa shule watapata mimba na kuharibiwa mitiririko yao ya masomo," alisema Ndagile.

Ndagile aliongeza licha ya kufanya utafiti na kubaini idadi ya wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, lakini takwa la uvaaji wa barakao na vitakasa mikono limewafanya waathirika wengi wa vitendo vya ukiukwaji wa haki kushindwa kufika kwenye vituo vinavyotoa haki kama vile Mahakama, Polisi Mabaraza ya Ardhi kutokana na kushindwa kumudu gharama za kununua vifaa hivyo.

Alisema vyombo vya kutoa haki vimekuwa vikisisitiza kesi nyingi ziwasilishwe kwa njia ya maandishi, hali ambayo inasababisha baadhi ya waathirika kushindwa kumudu matakwa hayo kutokana na ukata wa fedha ambazo zingetumika kupata huduma ya wakili ili aandike nyaraka hizo.

Ndagile alisema Mbepace wanaendelea kutoa elimu juu ya athari za vitendo vya ukatili kwa kutumia mitandao ya kijamii na redio, na kwamba wanashirikiana na taasisi za dini na kamati zilizoundwa kukabiliana na corona.



Mkuu wa Wilaya ya Kyela, mkoani Mbeya, Claudia Kitta (wa pili kushoto), akiangalia injini ya boti, iliyotolewa msaada na Mbunge wa Jimbo la Kyela, Dk. Harrison Mwakyembe, kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Nyasa, baada ya kukabidhiwa na Katibu wa Mbunge huyo, Aman Mwakipesile (wa pili kulia), wilayani humo mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Kyela, Hanta Mwakifuna. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Askofu aonya wanaombeza Magufuli

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

ASKOFU wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God TAG, Jimbo la Mbeya Kaskazini, Prof. Donald Mwanjoka, amewashauri wanasiasa ambao wanabeza hatua ya Rais John Magufuli kumtanguliza Mungu katika mapambano dhidi ya janga la corona badala ya kuutumia zaidi ushauri wa kitaalamu.

Prof. Mwanjoka alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ibada ya shukrani kwa Mungu baada ya kuwalinda na ugonjwa wa Covid-19 kama Rais Magufuli alivyoagiza kuwa maombi hayo yafanyike kwa siku tatu.

Alisema maono ya Rais Magufuli kumtanguliza Mungu katika vita vya corona yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuliokoa taifa kwa madai kuwa maagizo hayo yalitoka kwa Mungu.

"Wakati tunahitimisha ibada ya shukrani kwa Mungu wetu aliyetulinda na janga hili, naomba niwasihi Watanzania hususani baadhi ya wanasiasa ambao wanabeza jitihada za Rais wetu katika kumtanguliza Mungu katika vita hivi wanastahili toba," alisema na kuongeza:


"Maana uamuzi wa kiongozi wetu hakika ulikuwa wa ufunuo, sisi watumishi tulifurahishwa na tutaendelea kumuunga."

Naye Mchungaji wa Kanisa la Pentekoste lililopo Mji wa Mbalizi, Angetile Mwaiteleke, alisema tangu Aprili 15, mwaka huu Rais Magufuli atangaze maombi maalum ya kuliombea Taifa wachungaji na mashehe wamekuwa mstari wa mbele kufunga na kuomba.

Alisema maombi hayo yamesaidia janga la corona kupungua na kwamba wanayo imani siku moja ugonjwa huo utaondoka kabisa.

Licha ya kuendelea kumuomba Mungu na kumshukuru alishauri wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ikiwamo kufuata ushauri wa wataalamu wa afya kama vile kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni mara kwa mara na kuvaa barakoa.

Nao waumini wa kanisa hilo, walisema tangu Rais Magufuli atangaze maombi waliendelea kufunga na kuomba kwa saa 12 ili Mungu asikie kilio chao na kuwaepusha na corona.





## Spika aingilia kati waliosimamishwa kuvuja mitihani

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, ameitaka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kufuatilia suala la watumishi wa Wizara ya Elimu na kitengo cha mitihani ambao wamesimamishwa kazi kutokana na kuvuja kwa mitihani ya kidato cha pili.

Zubeir alisema huu ni mwaka wa tatu tangu watumishi hao waliposimamishwa kazi kwa tuhuma hizo, huku suala hilo likiwa katika hatua ya uchunguzi katika Jeshi la Polisi.

Alisema watumishi hao wanastahiki kujua hatima ya suala lao kwa sababu wanaishi na familia, na kwamba wanapita katika kipindi kigumu cha maumivu ya maisha.

''Nimesikitishwa na suala hilo ambalo limechukua miaka miwili, huku bado lipo katika Jeshi la Polisi kwa uchunguzi tu wakati wafanyakazi hao wakipata maumivu ya maisha...naiomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Mkurugenzi wa Mashtaka kulifuatilia zaidi ili wajue hatima yao," alisema.

Baadhi ya Wawakilishi wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali walisikitishwa na suala hilo kuchukua muda mrefu, huku haki za watumishi hao zikiwa hazijapata ufumbuzi.

Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliiomba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kulipatia ufumbuzi suala hilo kwa sababu watumishi hao wanapita katika kipindi kigumu cha maumivu ya maisha.

''Mheshimiwa Spika, kwa nini suala la waliosimamishwa kazi kwa tuhuma za kuvuja mitihani limechukua muda mrefu likiwa katika ngazi ya Jeshi la Polisi tu kwa ajili ya uchunguzi?" Alihoji na kuendelea:

"Mheshimiwa, unajua tumeshikilia maisha ya watu na kuyaweka katika wakati mgumu."

Mwakilishi wa Chukwani, Mwanaasha Khamis, alisema familia na wananchi wanaulizia suala hilo na kutaka lifikie tamati kuhuu uchunguzi wake kwani umechukua muda mrefu.

"Tukio hilo limetokea tangu mwaka 2018 na hadi sasa walimu hao wamesimamishwa kazi kwa ajili ya uchunguzi, ambao haujakamilika, sijui kwa nini?" Aliuliza.

Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Said Hassan Said, alikiri suala hilo kuchukua muda mrefu, huku likiwa katika hatua ya awali ya uchunguzi.

''Nakiri kweli hili suala lipo muda mrefu katika hatua ya uchunguzi, lakini naahidi kulifuatilia zaidi kujua hatima yake," alisema.

Hata hivyo, alisema kesi za aina hiyo zenye kuhitaji mambo mengi ili kuthibitisha ukweli wake na kufikishwa mbele ya Mahakama, zinahitaji ushahidi uliokamilika.

Aidha, alisema haki za watumishi hao hazitapotea na kama wakishinda kesi hiyo watarudishwa kazini na kulipwa haki zao zote zinazostahili.

# Wawakilishi wapewa jukumu kuelimisha corona majimboni

**Na Rahma Suleimman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wametakiwa kuendelea kutoa elimu ya kupambana na ugonjwa wa corona katika majimbo ya uchaguzi ili wananchi wawe salama na kuendelea na kazi za ujenzi wa taifa.

Hayo yalisemwa na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, wakati akiwakabidhi barakoa ambazo zimetokana na fedha walizochanga kwa ajili ya kuwasaidia wapigakura wao.

Alisema Zanzibar imepiga hatua kubwa ya kupambana na ugonjwa wa corona kwa sababu wananchi wake wamekuwa wakifuata masharti ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa huo.

Naibu Spika huyo aliwataka wawakilishi kuzisambaza barakoa hizo na kuzifikisha kwa wapigakura wao kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa.

"Barakoa hizi zinatokana na fedha zetu tulizochanga kwa ajili ya kuwasaidia wapigakura katika majimbo ya uchaguzi kuona kwamba wanakuwa salama na maambukizo mapya," alisema.

Aidha, alisema barakoa hizo pia wamewakabidhi wajumbe watatu wa Baraza la Wawakilishi wanaotoka katika vyama vya upinzani baada ya kutambua mchango wao mkubwa wa kuishauri serikali.

"Wapo wenzetu wawakilishi watatu kutoka katika vyama vya upinzani, ambao tumewapa mgao wa barakoa hizo ili wakazikabidhi kwa wanachama wao," alisema.

Wawakilishi hao ni Waziri wa Afya, Hamad Rashid Mohamed; Waziri asiye na Wizara Maalumu, Juma Ali Khatib pamoja na Said Soud.

Naye Mnadhimu wa Baraza la Wawakilishi aliwapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuonyesha moyo wa ujasiri kuchangia mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Nimefurahishwa sana na juhudi za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kukubali kuchangia Sh. milioni 33 na kutengeneza barakoa ambazo leo hii tunawakabidhi kwenda kutumika kwa wapigakura wetu," alisema.

Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Khatib, aliwapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka CCM kwa kuonyesha mapenzi na kutambua mchango wa wajumbe kutoka upinzani.

"Sisi Wawakilishi wa upinzani tunawapongeza kwa dhati Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka CCM kwa kutujumuisha sisi na kutupatia mchango wa barakoa ili tuwapelekee wanachama wetu katika mapambano ya ugonjwa huu," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamechangia Sh. milioni 33 kwa ajili ya kutengeneza barakoa ambazo zimekusudiwa kusambazwa katika majimbo ya uchaguzi ya Wawakilishi Unguja na Pemba.



Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo, Rajab Ali Rajab (kulia), akiongoza operesheni maalum ya kuwakamata wananchi wanaofanya biashara haramu ya pombe za kienyeji katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZEC yawaita wananchi daftari la wapigakura

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imewataka wananchi ambao hawajaorodheshwa katika daftari la kudumu la wapigakura kujitokeza ili kutumia haki yao ya kidemokrasia kuchagua viongozi katika uchaguzi mkuu.

Mwenyekiti wa ZEC, Jaji mstaafu Hamid Mahmoud, alisema hayo wakati akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa.

Alisema Tume imeamua kurudia usajili wa daftari la kudumu la wapigakura baada ya kubaini kwamba wapo wananchi wengi hawajaandikishwa katika daftari hilo kwa sababu mbalimbali.

Alizitaja sababu hizo ikiwamo baadhi ya wananchi kukosa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi ambavyo kwa mujibu wa sheria ya uchaguzi ni lazima kwa mtu atakayeandikishwa na hatimaye kupiga kura.

"Tume inakusudia kuanza zoezi la wapigakura wapya ambao hawakuandikishwa katika awamu ya kwanza Mei 30, ambapo wito wetu wananchi kujitokeza kutumia haki ya kidemokrasia kupiga kura uchaguzi mkuu ujao," alisema.

Alisema Tume imejipanga kuendesha uchaguzi huru na haki na wanachokifanya kwa sasa kuondosha dosari zote ambazo zinaweza kusababsiaha malalamiko katika uchaguzi huo.

Aliwataka watu watakaosajiliwa katika kipindi cha awamu ya pili ni wale waliofikisha umri wa kupiga kura miaka 18 kwa mujibu wa sheria ambao pia wanatakiwa kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi.

Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wameipongeza ZEC kwa kujenga mazingira ya uwazi zaidi ambayo yanatoa matumaini makubwa kwamba uchaguzi mkuu wa mwaka huu hautakuwa na dosari na kusababisha baadhi ya vyama kususia uchaguzi.

Katibu Mwenezi wa Chama cha Ada-Tadea, Rashid Mshenga, aliitaka Tume kuendesha uchaguzi huru ambao utamwezesha mshindi halali kushika dola.

# Serikali yawapa hadhari madereva malori corona

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka madereva wa malori nchini kuchukua tahadhari dhidi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa wa corona ikiwa ni pamoja na kuhakikisha wanakula vyakula ambavyo vitalinda kinga zao za mwili.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na baadhi ya madereva wa kampuni mbalimbali za malori zinazosafirisha mizigo nje ya nchi waliofika katika maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyoko Mabibo jijini Dar es Salam kwa ajili ya kupima virusi vya corona.

Waziri Ummy alisema ugonjwa wa corona bado upo ingawa maambukizo yamepungua na kuwataka wananchi kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya ikiwa ni pamoja na kuepuka mikusanyiko isiyokuwa ya lazima, kunawa mikono kwa maji tiririka kwa sabuni, kuvaa barakoa na kuzingatia umbali wa zaidi ya mita moja kati ya mtu na mtu.

"Nimefurahi kuwaona mko hapa kwa ajili ya kupima virusi vya corona kama mtakutwa hamna maambukizo ya ugonjwa huu mjitahidi kula matunda yakiwamo machungwa, mananasi, malimao, mboga za majani na tangawizi hii itawasaidia kinga zenu za mwili kuwa juu. Pia muwapo safarini mnapopata nafasi msisahau kupiga nyungu," Waziri Ummy alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa maabara hiyo, Ambele Mwafulango, alisema pamoja na kupima vipimo vya wagonjwa wengine, kwa siku wanawapima madereva 200 walioko mikoani.

"Kuna utaratibu maalum wa kuchukuliwa sampuli ambazo zinatumwa Dar es Salaam kwa ajili ya vipimo, majibu ya vipimo hivyo yanatoka baada ya saa 48 kama madereva hao watakutwa hawana maambukizo watapewa vyeti ambavyo vinatumika kwa siku 14 hii itawasaidia kwenda kupeleka mizigo nje ya nchi bila ya kupimwa tena katika nchi wanazokwenda," alisema.

Mwafulango alisema kabla madereva hao hawajafanyiwa vipimo vya corona, wanapimwa joto la mwili na wale ambao watakutwa lipo juu hupewa huduma ya haraka zaidi ukilinganisha na wale ambao joto lao la mwili huwa sawa.

"Madereva ambao tunawakuta hawana maambukizo ya ugonjwa wa corona tunawapa elimu ya kujikinga na ugonjwa huu wanapokuwa safarini siku zote.

"Katika maabara hii ya Mabibo tuna mashine mpya tano ambazo ndani ya saa 24 zinapima vipimo 1800 hii imetufanya kupima vipimo vingi zaidi ukilinganisha na ilivyokuwa katika maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii iliyoko ofisi za NIMR Dar es Salaam ambapo tulikuwa na mashine mbili ambazo zilikuwa zinapima vipimo 300 hadi 400 jambo ambalo lilikuwa linachelewesha utendaji wetu wa kazi," alisema Mwafulango.

Serikali imetenga utaratibu maalum kwa ajili ya madereva wa malori wanaosafirisha mizigo nje ya nchi ambao wanafanyiwa vipimo vya ugonjwa wa corona kabla ya kusafiri ili kuhakikisha hawana maambukizo na kuwaepusha kupata usumbufu ambao utajitokeza wanapokuwa safarini.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, akizungumza na madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, katika kikao maalumu cha Baraza la Madiwani kilichojadili na kujibu hoja za Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali (CAG). Kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Albert Msovela na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Abel Shija. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Watendaji waelekezwa elimu corona

**Yasmin Protace,** MKURANGA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga Mkoa wa Pwani, Philberto Sanga, amewaagiza watendaji wa kata zote zilizopo katika wilaya hiyo kwenda kutoa elimu ya afya ya uzazi, kwa wazazi na walezi wa wanafunzi wanaosoma shule za msingi na sekondari.

Lengo ni kuwaepusha na mimba zisizotarajiwa hasa kipindi hiki cha mapumziko ya kupisha janga la corona.

Sanga aliyasema hayo wiki iliyopita wakati wa uwasilishwaji wa taarifa za kata za robo ya tatu kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Alisisitiza kuwa anasikitishwa sana na baadhi ya wazazi wanaowaachia watoto wa shule kufanya biashara ndogo ndogo na wengine kutembea mitaani pasipokuwa na kitu cha maana wanacho kifanya ambacho kinaweza kuleta tija katika masomo yao.

Badala yake aliwataka wakae nyumbani wakijisomea, huku wakijiepusha na vitendo vitakavyoathiri elimu yao baada ya shule kufunguliwa.

Aidha, baadhi ya madiwani waliunga mkono agizo hilo na kusisitiza ya kuwa wazazi wawe makini na watoto wao ili kuepusha kuchukuliwa hatua za kinidhamu, na hatimae adhabu za vifungo au faini kwa wale wote watakaokwenda kinyume cha sheria za malezi ya watoto wadogo na wanafunzi.

Pamoja na kupokea agizo hilo baadhi ya madiwani walimpongeza Naibu waziri wa Mifugo na Uvuvi na Mbunge wa jimbo la Mkuranga Mh. Abdallah Ulega, kwa juhudi anazozifanya katika kuwaletea wananchi wa Wilaya ya Mkuranga maendeleo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mhandisi Mshamu Munde, aliwashukuru wakuu wa idara na vitengo kwa juhudi wanazozifanya za kusimamia miradi ya maendeleo, na aliwataka kusimamia ubora na viwango vya miradi yote inayoanzishwa katika wilaya ili iwe na hadhi chanya kwa jamii na maendeleo ya wilaya kwa ujumla.

# Nyamongo kulipwa fidia ya bil. 33/-

**Na Timothy Itembe,** MARA

ZAIDI ya wakazi 1,639 wa Matongo na Nyabichune eneo la Nyamongo wilayani Tarime, mkoani Mara vitaanza kunufaika na fidia ya Sh. bilioni 33.

Fidia hiyo imeanza kulipwa hivi karibuni na mgodi wa Barrick North Mara ikiwa ni utekelezaji wa maagizo ya Rais John Magufuli aliyoyatoa wakati wa ziara yake mkoani humo mwaka 2018 na kuagiza kulipwa fedha hizo.

Akizungumza wakati wa utoaji fidia na ugawaji wa hundi kwa wakazi hao, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliwataka kuhakikisha wenye haki ya kulipwa wanalipwa.

Aidha, ameiagiza Bodi ya Kampuni ya Twiga Corporation Limited, kuhakikisha inaufungamanisha mgodi huo na shughuli za wananchi kiuchumi ili waweze kunufaika na uwepo wa mgodi wake.

Pia, aliutaka mgodi huo kuangalia na kuzifanyia kazi changamoto za kijamii zinazowakabili wananchi wanaozunguka mgodi huo zikiwamo za maji, barabara na ili kujenga mahusiano mazuri na jamii hiyo.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Azzan, alisema wizara yake imejiridhisha kuhusu usalama wa taka sumu na kuongeza kuwa mara kwa mara umekuwa ukifanyika ukaguzi kuhakikisha maji hayo hayaathiri wananchi wanaozunguka mgodi huo.

Naye, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alisema utoaji fidia umechukua muda mrefu kwa sababu wananchi hawakuwa wakitoa taarifa sahihi na baadhi kutegesha na akatumia fursa hiyo kuwataka wananchi kutoa ushirikiano wa kweli kwenye masuala yote yanayohusu ulipaji fidia.

Kwa upande wake, Meneja Mkuu wa Migodi ya Barrick, Hilaire Diarra, alisema kampuni hiyo imeanza safari mpya ya amani, ufanisi wa pamoja kwa maendeleo ya jamii. Alisema kwa miaka mingi mahusiano kati ya mgodi na jamii hiyo yamekuwa siyo mazuri, lakini hivi sasa mgodi huo unaamini katika kuyajenga upya.

"Tumetembea miezi minne kufikia hapa, makinikia, ushuru, utafiti, vibali vya kazi, wafanyakazi wa nje, usajili wa jina la Twiga. Nakumbuka mara ya mwisho Waziri (Biteko) ulikuwa bado ukisisitiza suala la fidia liwe historia," alisema Diarra.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc), Dk. Samwel Gwamaka, alisema mamlaka hiyo inafanyia kazi malalamiko ya wananchi wanaozunguka migodi sambamba na kukagua iwapo taratibu za mazingira zinafuatwa.

## HABARI KIMATAIFA

# Mlipuko corona kuwa mbaya zaidi A. Kusini

**PRITORIA,** Afrika Kusini

RAIS wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, ametahadharisha kuwa hali ya mlipuko wa virusi vya corona inaelekea kuwa mbaya zaidi, wakati akitangaza kulegeza masharti ya kubaki nyumbani.

Ramaphona alisema zaidi ya watu 22,000 wamerekodiwa kuwa na maambukizo wiki iliyopita na kwamba sharti la kutotoka nje halijaondolewa moja kwa moja.

Rais huyo alitangaza kuwa kuanzia Juni Mosi, masharti zaidi yataondolewa.

**Tutarajie kuwa idadi ya watu walioambukizwa itaongezeka zaidi na kwa haraka, janga la corona Afrika Kusini litakuwa baya zaidi kabla ya hali kuwa nzuri.**

Ramaphosa alikuwa akizungumza baada ya kampuni ya madini nchini humo kusema kuwa wafanyakazi 164 katika mgodi wa dhahabu karibu na mji wa Johannesburg wamekutwa na maambukizo ya corona.

Mpaka sasa nchi hiyo imethibitisha vifo vya watu 429 vilivyotokana na maambukizo ya corona.

Alisema sharti la muda wa kurejea nyumbani halitakuwapo, biashara zaidi zitaruhusiwa kuendelea na shule zitafunguliwa.

Marufuku ya biashara ya pombe itaondolewa kwa idadi maalumu ya mauzo kwa ajili ya matumizi ya nyumbani pekee na kwa masharti ya siku maalumu na saa maalumu.

Rais Ramaphosa alisema marufuku ya biashara ya sigara itaendelea kuwapo kutokana na hatari za kiafya zinazotokana na uvutaji wake.

Pia alisema shule zitafunguliwa kwa awamu kwa sababu wanazingatia maendeleo ya watoto na kizazi chote cha watu wanaojifunza hawapaswi kuwa waathirika wa kudumu wa janga hilo.

"Hakuna mzazi atakayeshurutishwa kumpeleka mtoto shuleni kama watakuwa na wasiwasi kuhusu usalama wao shuleni," alisema.

Rais Ramaphosa amekuwa kwenye shinikizo kubwa akitakiwa kulegeza masharti ili kuufungua tena uchumi.

Hata hivyo, ameutahadharisha umma kuwa hali itakuwa mbaya siku za usoni.

"Tutarajie kuwa idadi ya watu walioambukizwa itaongezeka zaidi na kwa haraka, janga la corona Afrika Kusini litakuwa baya zaidi kabla ya hali kuwa nzuri," alisema.

Wiki iliyopita, wanasayansi walitahadharisha kuwa, kuna uwezekano wa takriban watu 40,000 kupoteza maisha nchini humo ifikapo mwishoni mwa mwaka.

Mgodi wa Mponeng ni mgodi mrefu zaidi kwenda chini kuliko mgodi mwingine wowote duniani. Operesheni zake ziliathiriwa baada ya watu 164 kubainika kuwa na maambukizo ya virusi vya corona.

Wengi kati ya waliobainika walikuwa hawaoneshi dalili zozote za kuwa na virusi hivyo.

Wote wametengwa, kwa mujibu wa wamiliki wa mgodi, AngloGold Ashanti. **BBC**



Brazil ni nchi ya pili duniani hivi sasa kwa kuwa na maambukizo mengi ya virusi vya corona baada ya Marekani. **PICHA MTANDAO**

# Trump apiga marufuku wasafiri wa Brazil

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amepiga marufuku wasafiri kutoka Brazil ikiwa ni katika kupambana na virusi vya corona.

Ofisa Habari wa Ikulu ya White House mjini Washington, Kayleigh McEnany, alisema kuanzia Alhamis wiki hii, watu wote wasio raia wa Marekani ambao wamekuwa nchini Brazil katika muda wa wiki mbili zilizopita, hawataruhusiwa kuingia Marekani.

Alisema hatua hiyo ni juhudi ya kuepusha maambukizo mapya kutoka nje ya nchi.

Marufuku hiyo haitawahusu raia wa Marekani wanaorejea nyumbani na pia wale wenye vibali vya kudumu vya kuishi nchini humo.

Brazil ambayo hivi sasa inavyo visa vipatavyo 367,000 vya corona na imerekodi vifo zaidi ya 22,000 kutokana na virusi hivyo, ipo katika nafasi ya pili kuwa na idadi kubwa ya maambukizo ya corona, ikitanguliwa na Marekani.

Licha ya hali hiyo, Rais wa Brazil, Jair Bolsonaro anaendelea kuubeza mlipuko wa janga la corona, akishikilia kuwa ni mafua ya kawaida.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Brazil, ilisema haikuipa umuhimu mkubwa marufuku hiyo ya safari ya Marekani, ikiitaja kuwa ni mchakato wa kawaida wa tahadhari. **DW**

## Netanyahu avituhumu vyombo vya sheria kula njama

**YERUSALEMU,** Israel

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amevishambulia vikali vyombo vya sheria vya nchi humo, akivituhumu kula njama ya kumuondoa madarakani na kujitaja kuwa kiongozi imara wa sera za mrengo wa kulia.

Netanyahu alisema hayo juzi alipofikishwa mahakamani katika kesi iliyokuwa ikisubiriwa kwa shauku kubwa. Amekuwa akiandamwa na shutuma za ufisadi kwa muda wa miaka mitatu na kesi hiyo iliahirishwa mwezi Machi kutokana na janga la corona.

Netanyahu amekuwa Waziri Mkuu wa kwanza aliyeko madarakani kufikishwa mahakamani tangu kuundwa kwa taifa la Israel zaidi ya miaka 70 iliyopita. **DW**

## Japan kuondoa tahadhari corona

**TOKYO,** Japan

WAZIRI Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, amesema hali ya tahadhari itaondolewa nchini humo kwa sababu taifa hilo limefaulu kudhibiti kuenea kwa virusi vya corona kwa muda wa miezi miwili.

Awali, Waziri anayehusika na kuupa nguvu mpya uchumi, Nishimura Yasutoshi, alisema jopo la ushauri limependekeza amri hiyo iondolewe.

Japan, ambayo ni taifa la tatu kiuchumi ulimwenguni imekuwa na visa 16,600 vya maambukizi na vifo 839.

Katika bara la Ulaya, nchi kadhaa za Umoja wa Ulaya, zinatarajiwa kulegeza zaidi masharti yaliyowekwa ya kukabiliana na virusi vya corona.

Idadi ya maambukizo ya virusi vya corona ulimwenguni imefika milioni 5.4 huku vifo vikiripotiwa kuwa 345,000. Nchini Marekani idadi ya vifo imekaribia 100,000. **DW**

# ARSENAL YAJITOSA KWA COUTINHO



**LONDON,** England

ARSENAL imeripotiwa kufungua mazungumzo na wakala wa kiungo wa Barcelona, Philippe Coutinho ili kumsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

Coutinho alikuwa na mkataba wa muda mrefu wa mkopo pale Bayern Munich, lakini miamba hao wa Bundesliga wamebainisha kwamba hawatamsajili kwa mkataba wa kudumu.

Maana yake ni kwamba, raia huyo wa Brazil atarudi Barcelona mwishoni mwa msimu huu, ambako inaonekana ni ngumu kwake kupata namba kwenye kikosi cha kwanza.

Coutinho alihamia Nou Camp akitokea Liverpool miaka mitatu iliyopita na ameshindwa kuwa kwenye kikosi cha kwanza na anaonekana kwamba ataondoka kipindi hiki cha majira ya joto.

Kwa mujibu wa Le10sport.com, Arsenal imejitosa kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, na wamefungua mazungumzo na wakala wake, Kia Joorabchian.

Kocha wa 'Washikabundi' hao, Mikel Arteta inaaminika kwamba ni shabiki mkubwa wa Coutinho, ambaye anaweza kuwa nguzo kubwa kwenye nafasi ya kiungo mshambuliaji.

# Boateng atumai kubaki Bayern

**MUNICH,** Ujerumani

JEROME Boateng anapanga majaliwa yake pale Bayern Munich kuliko kwenda sehemu nyingine kumalizia kipindi chake cha uchezaji soka, na amemsifia Hansi Flick.

Mlinzi huyo amekuwa akihusishwa na kuondoka pale kwenye dimba Allianz Arena kabla ya Flick kupewa nafasi ya ukocha akichukua mikoba ya Niko Kovac Novemba mwaka jana.

Mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2020-21, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, anahisi kuwa na uhakika kuhusu kumalizia maisha yake ya soka Bayern baada ya kuwa kwenye mipango ya Flick.

Hilo halikuwapo chini ya Kovac, lakini mabadiliko yamekuja tu na sasa Boateng hataki kuondoka hapo.

"Kabla ya Hansi Flick, tayari nilikuwa nafikiria kuhusu majaliwa yangu. Lakini wakati huu najihisi vizuri na nina uhakika nitabaki hapa," alisema Boateng akiiambia Welt am Sonntag.

Boateng amekuwa pale Bayern tangu alipowasili kutoka Manchester City mwaka 2011.

Aliongeza: "Nahitaji kocha anayeniamini na safu yake ya benchi la ufundi. Nimempata."





# Barca haimuwezi Martinez - Zamorano

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA haiwezi kumsajili nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez, kwa mujibu wa mshambuliaji wa zamani wa 'Nerazzurri' hao, Ivan Zamorano.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, Martinez ameripotiwa kuwaniwa na Barca na wapinzani wao kwenye LaLiga, Real Madrid baada ya kufunga mabao 18 katika mechi 33 alizocheza msimu huu.

Inter imeripotiwa kuwa tayari kumchukua nyota wa Paris Saint-Germain, Edinson Cavani kama mrithi wake, lakini Zamorano "hana shaka" Martinez atabaki pale San Siro msimu ujao kutokana na matatizo ya kifedha baada ya mlipuko wa virusi vya corona.

"Kwa hakika kabisa natumaini Lautaro atabakia Inter. Yeye ni kijana mwenye umri wa miaka 22, Cavani ni mkubwa kwake kwa miaka 11 na ana uzoefu katika klabu kadhaa tofauti.

"Lakini ujio wa Cavani hauna athari yoyote kwa Lautaro," alisema akiiambia televisheni ya nchini Mexico ya MisionTUDN.

"Barcelona wana matatizo ya kiuchumi ambayo hauruhusu kumsajili Lautaro, hivyo kwa maoni yangu atabakia, sina shaka kwa hilo."

# Mane au Mbappe kutua Real Madrid

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid imeweka wazi kwamba, kati ya Sadio Mane au Kylian Mbappe mmoja wao watamsajili kipindi hiki cha majira ya joto.

Kocha, Zinedine Zidane anahitaji kuongeza makali kwenye safu yake ya ushambuliaji katika chama lake la 'Los Blancos' ili kuwa moto zaidi msimu ujao na sasa mezani kuna majina mawili ya kuanza nayo wakati dirisha la majira ya kiangazi litakapofunguliwa.


Majina hayo ni Mane na Mbappe, lakini kwa mujibu wa ripoti zilizopatikana kutoka Hispania ni kwamba, Real Madrid imeamua kuwekeza nguvu yao kubwa kwenye kumnasa staa wa Liverpool, Mane na kuachana na Mbappe katika uhamisho wa mwaka huu.

Madrid wamegundua kwamba itakuwa ngumu kuwashawishi Paris Saint-Germain na kupata huduma ya Mbappe mwaka huu, huku wakiamini kwamba kwenye dirisha la uhamisho wa majira ya kiangazi la mwakani watampata mchezaji huyo kwa dau dogo zaidi.

PSG hawataki kabisa kuzungumza kuhusu kumuuza staa wao Mbappe kwenda Madrid mwaka huu na sasa Zidane amegeuza kibao kwa Mane, anayetajwa kuwa na thamani ya pauni milioni 131.

Na sasa Madrid wamepanga kumchukua Mane mwaka huu na mwakani watakamilisha dili la kunasa huduma ya Mbappe. Mabosi wa Real Madrid wanachokiamini ni kwamba, ni wao tu ndio watakaomshawishi Mane kubeba virago vyake na kuachana na miamba hiyo ya Anfield.

France Football limeshatoa ripoti likidai kwamba Mane mwenye umri wa miaka 28, amekuwa hana furaha huko Anfield baada ya kocha Jurgen Klopp kutumia nguvu nyingi kupigania Virgil van Dijk abebe tuzo ya Ballon d'Or kuliko yeye.







# DAVID LUIZ KUSTAAFIA BENFICA

**LONDON,** England

MLINZI wa Arsenal, David Luiz amefichua kwamba, hatamalizia soka lake katika klabu hiyo ya jiji London, na kwamba nia yake ni kustaafia Benfica ya Ureno.

Luiz mwenye umri wa miaka 33, amedai kuwa angependa amalizie soka la ushindani akiwa anachezea klabu yake ya moyoni Benfica ambayo ndio iliyomuibua.

Beki huyo alisema kuwa hawezi kuficha mahaba aliyonayo kwa Benfica na anatamani kurejea tena kwenye klabu hiyo aliyoichezea kuanzia 2007 hadi 2011 baada ya kujiunga nayo akitokea Vitoria ya Brazil.

"Siku zote nimekuwa nikisema kuwa nitapenda kumalizia maisha yangu ya soka pale Benfica.

Katika mpira wa miguu kila kitu kinabadilika. Kilicho cha kweli leo kinakuwa cha uongo kesho lakini kwangu haiko hivyo.

Ninaipenda Benfica. Ndoto zangu ni kuwapo kiwanjani nikiwa na rangi zao. Kwa yote niliyoishi na kuwaza, kwa kile kilichoifanya Benfica kuwa maishani mwangu na kwenye historia yangu, kwa kila kitu, Benfica ni kubwa kuliko mchezaji yeyote," alisema Luiz.

Luiz ametoa kauli hiyo licha ya hamu ya kocha wa Arsenal, Mikel Arteta kutamani kuendelea kubakia naye klabuni akikoshwa na sifa za uongozi alizonazo.

# Barcelona yamkomalia De Ligt amrithi Umtiti

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imekataa kuondoa uwezekano wa kumsajili mlinzi wa kati wa Juventus, Matthijs de Ligt.

Miamba hiyo ya Hispania, sambamba na Manchester United, kwa muda mrefu wamekuwa wakimfukuzia Mdachi huyo tangu kwenye dirisha la majira ya kiangazi la mwaka jana, lakini Juventus ilishinda kwenye mbio hizo za kunasa huduma yake akitokea Ajax. De Ligt amecheza mechi 27 tu Juventus msimu huu, lakini kiwango chake kimezua maswali na sasa staa huyo anaweza kufunguliwa mlango mwishoni mwa msimu ujao.

Barca waliripotiwa kuweka mezani pauni milioni 66 ili kunasa saini ya beki huyo mwaka jana, lakini Juventus iligomea ofa hiyo, na sasa miamba hiyo ya Nou Camp inapambana kuhakikisha wanamnasa Mdachi huyo.

Kikosi hicho cha Quique Setien kimeripotiwa kwamba, kitaingia sokoni kusaka beki wa kati mpya kuwapa changamoto Clement Lenglet na Gerard Pique, huku Samuel Umtiti akidaiwa kwamba atafunguliwa mlango wa kutokea.

Real Madrid nayo ipo vitani kuisaka saini ya De Ligt, licha ya kusaini mkataba wa miaka mitano wakati alipotua Juventus Julai mwaka jana.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED YAGONGA UKUTA KWA IGHALO

## Wachina wamwongezea mshahara hadi pauni 400,000 kwa wiki, wataka...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imegonga 'ukuta wa matofali' katika jaribio lao la kutaka kumwongezea muda wa mkopo Odion Ighalo huku ikiwa imesalia wiki moja tu kabla ya mkataba huo kumalizika.

**Klabu ya Shanghai Shenhua imekataa maombi ya United kuendelea kukaa na Ighalo pale Old Trafford kwa miezi mingine mitatu na wanamtaka mshambuluaji huyo wa Nigeria kujiunga nao kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu ya China, Super League.**

Kama United hawataweza kufanya mazungumzo ya haraka, Ighalo atarudi katika klabu ya Shanghai wakati mkataba wake utakapomalizika Jumatatu akiwa ameshacheza mechi yake ya mwisho kwa kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye alianza mazoezi na kikosi cha United pale Carrington wiki iliyopita, angependa kumaliza msimu akiwa England baada ya kufunga mabao manne katika mechi nane kabla ya mlipuko wa virusi vya corona.

Lakini Shanghai ndio wenye neno la mwisho kuhusu Ighalo, ambapo wamempa ofa mpya mchezaji huyo wa zamani wa Watford ya miaka miwili hadi 2024, huku akiwa ameongezewa mshahara hadi pauni 400,000 kwa wiki.

United ililipa pauni milioni tatu kama ada ya Ighalo mwishoni mwa Januari na wamekuwa wakichangia katika mshahara wake wa pauni 130,000 kwa wiki, ingawa hajacheza kwa miezi miwili na nusu.

Awali mkataba wake wa mkopo ulikuwa hadi Mei 31, na Man United wanataka kumbakisha Ighalo hadi mwishoni mwa Agosti wakati msimu wa sasa utakapomalizika, lakini Shanghai wamekataa majadiliano ya hilo.

Licha ya uvumi kudai kuwa klabu hiyo ya nchini China kujiandaa kuuuza mchezaji huyo kwa pauni milioni 20, mkataba wa kudumu haujajadiliwa.

Hakuna mazungumzo hadi mwanzoni kwa dirisha jipya la usajili, ambalo linatarajiwa kufunguliwa Agosti hadi Oktoba.

United imebadilika tangu ujio wa Ighalo miezi mitatu iliyopita akirithi mikoba ya Marcus Rashford ambaye alikuwa majeruhi kutokana na kuumia mgongo.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KWA COUNTINHO

KLABU ya Arsenal inatarajiwa kuanza mazungumzo na wakala wa kiungo wa kati wa Barcelona, Phillipe Coutinho. Mchezaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 27, amekuwa akicheza kwa mkopo kule Bayern Munich, lakini klabu hiyo haiko tayari kulipa paundi milioni 105 ili kumsajili.***(Le10sport)***

### HIGUAN AGOMEWA EPL

MSHAMBULIAJI wa Juventus, Gonzalo Higuain mwenye umri wa miaka 32, huenda akarudi Ligi Kuu ya England, kwani anawaniwa na Newcastle na Wolves. ***(Express)***

### WERNER ASOGEZEWA UNITED

NYOTA wa RB Leipzig Timo Werner mwenye umri wa miaka 24, anahusishwa na uhamisho wa kujiunga na Liverpool, na aliyekuwa mchezaji wa zamani wa Manchester United, Owen Hargreaves anahisi kwamba uhamisho wa klabu hiyo ya Old Trafford ungekuwa bora zaidi kwa mchezaji huyo. ***(Star)***

### JIMENEZ LULU USAJILI

MSHAMBULIAJI wa Wolves, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 29, akiwa na thamani ya pauni milioni 57, ananyatiwa na Manchester United, Arsenal na Real Madrid. ***(Tuttosport)***

### AUBAMEYANG ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inafanya mazungumzo na Arsenal katika jaribio la kumsainisha mashambuliaji wa klabu hiyo, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 30, kwa pauni milioni 34. ***(Todofichajes)***

### JUVE KUIPIKU MADRID

JUVENTUS inataka kuipiku Real Madrid katika usajili wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 19, katika kipindi cha dirisha la majira ya joto kwa kutoa pauni milioni 67. ***(Tuttosport)***

### BARCA KUMUUZA DEMBELE

KLABU ya Barcelona iko tayari kumuuza mashambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 23, kwa dau la pauni milioni 37. Klabu hiyo ya Hispania ililipa pauni milioni 137 kumnunua raia huyo wa Ufaransa miaka mitatu iliopita. ***(Mirror)***

### TRAORE KUITOSA OFA LIVER

WINGA Adama Traore mwenye umri wa miaka 24, ameshauriwa kuipuuza Liverpool na kubakia katika klabu ya Wolves kwa msimu mwingine, ushauri huo ukitolewa na mchezaji wa zamani wa Sheffield United, Michael Brown. ***(Star)***

### MATONDO AIKATAA UNITED

WINGA wa Wales na FC Schalke, Rabbi Matondo mwenye umri wa miaka 19, amesema hana mpango wa kuondoka katika klabu hiyo ya Ujerumani, licha ya kuhusishwa na Manchester United. ***(Manchester Evening News)***

### MAN CITY YAITOSA BARCA

KLABU ya Barcelona imetoa ofa kwa nyota wa Manchester City, Nelson Semedo, mwenye umri wa miaka 26, ikiwa sehemu ya kutaka kumsajili mlinzi wa kulia Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 25, lakini City imeonyesha haina mpango huo. ***(Marca)***

HABARI MICHEZO

# Ruvu yalalamikia Ligi Kuu ya vituo

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Ruvu Shooting imelalamikia hatua Ligi Kuu Tanzania Bara kuchezwa kituo kimoja na kusema kuwa kimahesabu gharama itakuwa kubwa zaidi kuliko mfumo ule wa nyumbani na ugenini.

Msemaji wa klabu hiyo, Masau Mbwire alisema kuwa wao hawakuona ubaya wowote wa timu kucheza nyumbani na ugenini na hasa kwa upande wa gharama.

"Ikumbukwe kuwa hapa mimi nashauri tu kwa sababu serikali imeshasema kuwa ligi ni ya vituo. Hakuna mtu anayeibishia serikali, ikisema imesema. Ila serikali huwa inapokea ushauri. Ushauri wangu ni kwamba naona kabisa kuwa kukaa kituo kimoja gharama itakuwa kubwa zaidi kuliko ile ya nyumbani na ugenini," alisema Masau na kuongeza:

"Mimi ni mwalimu wa hesabu, ni kwamba kwenye Jiji la Dar es Salaam hoteli yenye hadhi ya chini chumba ni Sh. 40,000 kwa siku, huku karibu kila timu ikiwa na wachezaji 30 na viongozi kwa siku zote ambazo ligi inachezwa, chakula cha asubuhi mchana na jioni, lakini kwa Dar es Salaam ninavyoijua hakuna kiwanja cha bure, kiwanja cha bei rahisi ni laki moja, ukijumlisha vyote hivyo gharama zitakuwa kubwa sana," alisema msemaji huyo.



Alisema kwa idadi ya michezo ya ugenini ambayo Ruvu Shooting ilibakiza, ingetumia gharama ndogo tu kwenda na kurejea mkoani Pwani ambako ndiko makao makuu ya klabu hiyo.

Hata hivyo, serikali imetoa kiasi cha pesa kwa ajili ya kupunguza gharama kwa klabu za Ligi Kuu, Daraja la Kwanza Tanzania Bara na la Pili.

Ligi Kuu ambayo ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, hadi inasimama Ruvu Shooting ipo nafasi ya 11 ikiwa na pointi 39 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoongozwa na Simba yenye alama 71 ikifutiwa na Azam ikiwa na pointi 54 baada ya timu zote kushuka dimbani mara 28.

Tayari serikali imeruhusu ligi hiyo kuweza kurejea kuanzia Juni Mosi, mwaka huu baada ya kujiridhisha na kupungua kwa takwimu za wagonjwa ikiwa ni pamoja na kasi ya maambukizo ya virusi vya corona kushuka.

# NAMUNGO FC YALIA KOCHA MKUU KUKWAMA RWANDA

**Na Saada Akida**

HUKU Serikali ya Tanzania ikiwa imeruhusu ligi za soka nchini kurejea muda wowote kuanzia Juni Mosi, mwaka huu, hofu ya kumpata Kocha wao Mkuu, Thierry Hitimana, kabla ya Ligi Kuu kuanza, imetanda kwa uongozi wa Klabu ya Namungo.

Ligi Kuu Bara ilisimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona vinavyoendelea kuitesa dunia, lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, ameruhusu irejee baada ya kuridhishwa na kupungua kwa maambukizo nchini na kasi ya wagonjwa walioambukizwa kupona.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu, alisema licha ya Tanzania kufungua viwanja vya ndege, bado kwao ni mtihani mkubwa kwa sababu ya kocha wao huyo kukwama kuja nchini kutokana Rwanda kutofungua mipaka.

**Alisema kocha wao atashindwa kufika mapema kutokana na Rwanda kuzuia mtu na vyombo vyote vya usafiri kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kutokana na kuendelea kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona.**

"Zuio la Rwanda bado linatuumiza kichwa kwa sababu kocha wetu anaishi mkoa mbali na uwanja wa ndege pia hata katika mipaka imefungwa, hivyo anatakiwa kusafiri mikoa mitatu hadi kufika kupata usafiri.

"Lakini kutokana na zuio hilo, lililomkwamisha kurejea mapema, pia hatujajua wanafungua lini, hilo linatuumiza kichwa juu ya uwapo wake na kuiwahi ligi," alisema Zidadu.

Alisema tayari timu yao imeanza mazoezi chini ya kocha msaidizi, Mrundi Godfrey Okoko ambaye hakwenda kwao kipindi cha mapumziko ya corona.

Aidha, alisema wanafanya utaratibu wa wachezaji wao wawili, Bigirimana Blaise na Sytve Nzigamasabo kutoka Burundi waweze kuwasili ndani ya siku mbili hizi na kupima afya kabla ya kujiunga na wenzao.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Namungo ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi 50 zilizotokana na kushuka dimbani mara 28.




Mshambuliaji wa kimataifa wa Tanzania na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta akiwa mazoezini na klabu yake ya Aston Villa kujiandaa kumalizia Ligi Kuu ya England iliyosimama tangu katikati mwa Machi kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona (Covid-19). **PICHA: MTANDAO**

# *Klabu Ligi Kuu Z'bar zaiangukia serikali*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KLABU zinazoshiriki Ligi Kuu ya Zanzibar, zimeiangukia serikali zikiomba kusaidiwa gharama za kumalizia ligi pindi itakaporuhusu michezo kurejea visiwani hapa, kutokana na kukabiliwa na changamoto kubwa za kifedha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Klabu za Ligi Kuu Zanzibar, Haji Issa Kidali, alisema hatua hiyo imefikiwa baada ya makatibu wa klabu kukutana na kujadili hatima ya ligi hiyo ambayo imesimama kutokana na Ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Alisema klabu kwa pamoja katika maadhimisho yao, zilieleza kwa sasa zinakabiliwa na hali ngumu ya kifedha, hivyo iwapo serikali itatoa tamko la kuendelea kwa ligi ni vema Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), liangalie namna ya kuzisaidia.

Kidali alisema klabu zote za Ligi Kuu zipo tayari kumalizia ligi hiyo ambayo imebakia michezo kadhaa endapo zitasaidiwa fedha ili kupunguza changamoto ya ukata kulingana na ratiba itakayotolewa na shirikisho hilo.

"Tumekaa na klabu zinazocheza Ligi Kuu ya Zanzibar, klabu zote zipo tayari kumaliza msimu, lakini changamoto kubwa ipo katika uendeshaji wa timu zao kwa kipindi hiki na hii inatokana na changamoto ya fedha ya kurudi tena katika ligi, huku tukiwa na muda mchache kabla ya kuingia msimu mpya," alisema.

Hata hivyo, alisema hatua hiyo ya kuomba kusaidiwa pia inatokana na Ligi Kuu ya Zanzibar kutokuwa na mdhamini, hivyo klabu kutumia gharama zao katika suala zima la kuziendesha timu zao.

# Michezo

Jumanne Mei 26, 2020

Nipashe




United yagonga ukuta kwa Ighalo

UKURASA 22

PUMZIKA KWA AMANI...




Aliyekuwa Katibu na Beki 'kisiki' wa zamani wa Yanga, Lawrence Mwalusako (kushoto) enzi za uhai wake, akimkabidhi Mrisho Ngassa jezi aliposaini kurejea Jangwani Mei 20, mwaka 2013 akitokea kwa mahasimu wao, Simba, alipokuwa anacheza kwa mkopo akitokea Azam FC. Mwalusako alifariki jana asubuhi katika Hospitali ya Muhimbili. **PICHA: MAKTABA**

## Mwalusako alivyozua majonzi mazito Yanga

**Na Saada Akida**

NI zaidi ya majonzi katika soka la Tanzania, hususan kwa Klabu ya Yanga baada ya aliyekuwa Katibu Mkuu na mchezaji wa zamani wa timu hiyo na Taifa Stars, Laurence Mwalusako kufariki dunia jana asubuhi wakati akipigania uhai wake katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili alipokuwa amelazwa kwa matibabu.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, msemaji wa familia ya marehemu, Hamis Chande, alisema Mwalusako alikuwa akisumbuliwa sana na shinikizo la damu na ndio ugonjwa uliosababisha mauti kumkuta hospitalini hapo.

Alisema awali alikuwa akiumwa na kupelekwa kutibiwa katika Hospitali ya Sinza Palestine kabla ya wiki iliyopita kuhamishiwa Muhimbili.

"Baada ya kufika Muhimbili alipelekwa Moi, aligundulika kichwani kunavuja damu na kuingia katika ubongo na alifanikiwa kufanyiwa upasuaji haraka, lakini hadi umauti unamkuta presha haikuwa nzuri kwake," alisema.

Kuhusu taratibu za mazishi, Chande alisema, mwili wa marehemu utasafirishwa kesho, Jumatano kuelekea Kyela, Mbeya na mazishi kufanyika kesho yake, Alhamisi.

Kwa upande wa Yanga, iliungana na wadau wa soka nchini kumlilia Mwalusako kwa Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Dk. David Ruhago, kueleza kuwa watashiriki kikamilifu kwenye msiba huo wa Mwalusako ambaye enzi za uchezaji wake alikuwa beki mahiri aliyemudu kucheza nafasi zote za ulinzi.

# Simba kamili kwa ubingwa

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Majembe yote ndani, daktari asema yamekamilika kwa lolote uwanjani, huku...

WAKATI wakitarajia kuanza mazoezi rasmi Jumatano kujiandaa na kuhitimisha mechi zao 10 zilizosalia za Ligi Kuu Bara, Daktari wa Klabu ya Simba, Yassin Gembe, amesema wachezaji wa timu hiyo wote wako 'fiti' kiafya tayari kuendelea na ligi hiyo ili kutetea taji lao.

**Kuanza mazoezi kwa Simba kunatokana na serikali kuruhusu Ligi Kuu, Kombe la FA, Ligi Daraja la Kwanza na la Pili kurejea siku yoyote kuanzia Juni Mosi, mwaka huu baada ya kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Covid-19, ambao unaendelea kuitesa dunia hadi leo.**

Hata hivyo, Serikali ya Tanzania imefikia hatua hiyo ya kuruhusu ligi hizo kurejea baada ya kujiridhisha na kasi ya maambukizo kupungua nchini ikiwa ni pamoja na takwimu za wagonjwa walioambukizwa virusi vya corona kuendelea kushuka kila uchao kutokana na kupona.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Gembe alisema amewasiliana na wachezaji wote ambao kwa sasa wako mapumzikoni kupisha janga hilo la corona, ambao kwa sasa wanafanya mazoezi binafsi na kueleza hali zao kiafya wote ni nzuri na wapo tayari kurejea kufanya mazoezi ya pamoja kabla ya ligi hiyo kuanza.

Hata hivyo, alisema wameandaa utaratibu maalum wa kuwapima wachezaji wote baada ya kurejea kabla ya kuanza mazoezi ya pamoja.

"Baada ya wachezaji kurejea mazoezini, watapimwa kuangalia hali zao za kiafya ili kujiridhisha tena kama kipindi walichokuwa mapumziko hawajapata madhara yoyote.

"Nimewasiliana nao wote wako vizuri na wanaendelea na mazoezi binafsi huko walipo kulingana na programu tulizowapa, wakirudi tena tutawapima kujua hali zao katika muda waliokuwa mapumzikoni," alisema Dk. Gembe.

Juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingisa alithibitisha kuwa kikosi cha mabingwa hao watetezi kitaanza mazoezi Jumatano baada ya kumalizika kwa Sikukuu ya Eid jana.

Mazingisa alisema wachezaji wote walio nje ya nchi watawasili ndani ya muda kabla ya mazoezi ya timu hiyo kuanza.

"Wachezaji wetu wote ambao wapo nje ya Tanzania, tunawasiliana nao na mmoja kati ya hao atakuwapo nchini Jumatatu [jana]. Wengine tunatarajia watakuwapo nchini kabla hatujaanza mazoezi," alisema.

Wachezaji wa Simba waliokuwa makwao nje ya nchi ni mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere, kiungo Mzambia Clatous Chama, winga Mkenya Francis Kahata na kiungo Msudan Sharaf Eldin Shaiboub.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Simba ndiyo iliyoko kileleni mwa msimamo ikiwa na alama 71 baada ya kucheza mechi 28 sawa na Azam FC iliyopo nafasi ya pili na pointi zake 54, tatu mbele ya Yanga inayofuata lakini ikiwa nyuma kwa mchezo mmoja.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042